# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

## Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 21 Juni, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae!

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba *style* mpya. *(Kicheko)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Waliondoka Ukumbini)*

**NAIBU SPIKA**: Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Salome Wycliff Makamba, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Chegeni.

Na. 399

### Wafanyakazi wa Migodini Kufukuzwa Kazi Kiholela

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y MHE. SALOME W. MAKAMBA)** aliuliza:-

Wafanyakazi wa migodi ya uchimbaji wa madini hufukuzwa kazi kiholela bila kulipwa fidia stahiki kutokana na ulemavu na magonjwa yanayosababishwa na vitendea kazi hatarishi wakati wakiwa kazini.

(a) Je, Serikali iko tayari kuzuia kuingizwa nchini vitendea kazi hatarishi na kufunga migodi ambayo ina wahanga wengi na ulemavu na magonjwa yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kutumia Sheria ya Fidia Na. 20 ya mwaka 2008 ili wafanyakazi wa migodini walipwe fidia stahiki wanapopata ulemavu au magonjwa wanapokuwa kazini badala ya Sheria ya Fidia ya mwaka 2002? na

(c) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa waajiri wanaowatelekeza wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazini na kukataa kuendelea kulipa gharama za matibabu yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia taasisi zake na sheria mbalimbali za nchi inao utaratibu madhubuti wa kudhibiti uingizwaji wa bidhaa zisizo na ubora pamoja na vitendea kazi hatarishi kwa afya za wafanyakazi mahali pa kazi ikiwemo migodini.

Aidha, Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, imeipa mamlaka Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi kukagua vitendea kazi vinavyotumika mahali pa kazi ikiwa ni pamoja na migodi na kupima afya za wafanyakazi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Namba 20 ya mwaka 2008 ilitungwa ili kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara au kufariki wakiwa kazini, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa migodini wanaopata ajali.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria namba 20 itaanza kutoa rasmi fidia kwa wafanyakazi tarehe 1/7/2016. Kipindi hiki waajiri wote waendelee kutumia Sheria Na. 263 kuhakikisha wafanyakazi wanahudumiwa na kulipwa wawapo kazini. Aidha, Serikali inatoa onyo kwa waajiri ambao hawataki kutenda haki ya kuwalipa fidia kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Chegeni, swali la nyongeza.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni naomba ukae, Taarifa Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona neno wahanga libadilishwe katika *Hansard*, hili neno wahanga lina maana ni watu wanojivisha mabomu na kwenda kujitoa mhanga. Hapa neno linalopaswa kutumika ni waathirika. Kwa hiyo, neno wahanga sio neno zuri kutumika, ni hilo tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel hilo itabidi kuliangalia. Tutaliangalia ndipo tulifanyie maamuzi kwa sababu sasa unampa taarifa. Ni lazima tuliangalie kwa muktadha huu kama ni kweli tunatakiwa kutumia neno waathirika ama wahanga halafu tutalifuta wakati huo. Mheshimiwa Chegeni swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa waathirika wengi wa ulemavu, kama alivyosema Mheshimiwa Amina Mollel, katika migodi hii wanapata matatizo mengi sana wanapojikuta kwamba wanapoteza viungo vyao au wanapata ulemavu wakiwa kazini; na kwa kuwa waajiri wengi na hasa migodi hii wamekuwa hawalipi fidia wafanyakazi hawa wanaopata matatizo, na Sheria Namba 20 ambayo inaanza kutumika kuanzia mwezi ujao Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba ndiyo itaanza kushughulikia masuala haya.

Je, kwa wale waajiri ambao wamekaidi kwa muda mrefu, Serikali inatoa tamko gani ili kusudi wafanyakazi hawa ambao wameumia wakiwa kazini waweze kupata fidia zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la msingi Mheshimiwa Mbunge anauliza Serikali inachukua hatua gani au inatoa tamko gani kwa waajiri wote ambao wanakaidi kuwafidia wafanyakazi ambao wameathirika kutokana na magonjwa yanayotokana na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Sheria Namba Nane ya mwaka 2008 ambayo imeunda Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi kupitia kifungu cha tano cha sheria hiyo itaanza kufanya kazi tarehe 1 Julai, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa na maudhui ya Sheria hii ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wale ambao wamepata *occupation diseases* wanatibiwa kupitia mfuko huu; na wale ambao watakuwa wamepata ulemavu uliosababishwa na shughuli za kazi na wenyewe wanaweza kufidiwa au kupata mataibabu kutokana na aina ya ugonjwa walioupata kutokana na ripoti ya madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali sasa inafanyaje? Katika mazingira haya kumtaka mwajiri atimize wajibu wake uko utaratibu ambao uko kwa mujibu wa sheria ambao umewekwa ya kwamba waajiri wote watatakiwa kwanza kuwasilisha michango yao kwa mujibu wa sheria ambapo Sekta Binafsi watatakiwa kuchangia asilimia moja ya *wage bill* ya kila mwezi, na katika sekta ya umma vilevile asilimia 0.5. sasa kwa wale ambao watakaidi kuchangia maana yake ni kwamba kwanza sheria inasema watatozwa fine ya riba ya asilimia 10 ya kile ambacho wamekichelewesha, lakini pili watapelekwa pia mahakamani na wakithibitika kwamba wameshindwa kuwasilisha michango hiyo adhabu ni kuanzia shilingi milioni 50 au pia kifungo kisichopungua miaka mitano mpaka kumi cha mkuu wa taasisi hiyo.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali fupi la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wafanyakazi hasa vijana kufukuzwa kazi kiholela, kutokulipwa stahiki pindi wapatapo ajali kazini, kulipwa ujira mdogo sana wa shilingi 4,500 kwa kutwa ya siku, kufanyishwa kazi kwa muda mrefu kinyume cha sheria na taratibu za nchi lipo pia katika Wilaya yangu ya Mkuranga.

Je Serikali ina mpango gani wa kuwalinda vijana hawa wafanyakazi ili waweze kazi zao kuwa ni kazi zenye staha? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali kupitia Wizara ya Kazi tumekuwa tukisimamia sana Sheria Namba Sita ya mwaka 2004 ambayo imetoa haki na wajibu kwa wafanyakazi lakini na kwa waajiri pia. Sheria hii imetusaidia sana kutatua migogoro mingi mahali pa kazi, hasa pale inapoonekana sheria hii imekiukwa Serikali imekuwa ikichukua hatua stahiki kama ambavyo imekuwa ikionekana katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikija katika swali lake la msingi sasa ya kwamba Serikali tunawalindaje hawa ambao wanafukuzwa kazi kiholela hasa pale wanapoonekana wamepata ulemavu wakiwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kupata ulemavu ukiwa kazini sio kigezo cha *dismissal* na kwamba waajiri wote ambao wamekuwa wakikiuka taratibu hiyo ya sheria, sisi kama mamlaka ambayo tunasimamia sheria hizi kazi tumekuwa tukitoa elimu, lakini na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu ya kwamba tumekuwa tukiendelea kufanya kaguzi nyingi sana za kazi kwa lengo la kubaini haya mapungufu na tumekuwa tukichukua hatua pindi inapobainika kwamba mwajiri amekiuka sheria hizi. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutaendelea kusimamia Sheria Namba Sita ya mwaka 2004 kuhakikisha kwamba tunalinda haki za wafanyakazi na wafanyakazi hawa basi wasipoteze haki zao zile za kuwa wafanyakazi kwa kufukuzwa tu kiholela na mwajiri; na sisi tutahakikisha kwamba waajiri wote wanafuata sheria za nchi zinavyoelekeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa swali la msingi limeeleza jinsi watumishi wa migodini wanavyofukuzwa kazi kiholela, pengine wakifanya kazi kwa miaka minane, saba wanafukuzwa kutokana na magonjwa mbalimbali, na Serikali imeondoa fao la kujitoa kwenye Mifuko ya Jamii ikiweka masharti kwamba mpaka miaka 55.

Je, hawa waliofukuzwa kazi wakiwa na miaka tisa na umri wa miaka 40 wanapataje fao lao kwa kusuburi miaka 50 Maana watakuwa na miaka 100?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Hifadhi ya Jamii ambayo inaongoza masuala mazima ya Hifadhi ya Jamii katika nchi yetu ya Tanzania inaendana na Katiba ya nchi kifungu cha 11(1) ambacho Katiba ya nchi yetu inataka jamii kuangalia utaratibu mzima wa kuweka hifadhi ya wananchi na hasa pale wanapofikia umri wa uzeeni ama wanapopata matatizo mengine yoyote. Kwa hiyo, sera hiyo imekuwa ikituongoza kuunda mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kutoa kinga wakati wa uzeeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumepata matatizo ya namna moja ama nyingine. Kadiri uchumi wa Tanzania ulivyoendelea kukua kumeongezeka sekta za kiuchumi ambazo unapata picha kabisa kwamba wafanyakazi ambao wamekuwa wakiajiriwa katika sekta hizo ni lazima watafanya kazi kwa muda mfupi sana, kama katika sekta za migodi, sekta za mashamba na sekta nyinginezo na hivyo basi kumekuwa na namna moja ama nyingine ya kuonekana kabisa kunahitajika kupitia tena sera ya Hifadhi ya Jamii, na kupitia sheria zetu ambazo zinaongoza Mifuko ya Hifadhi ya Jamiii ili kuyapitia mafao yanayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kusudi la kufanya hivyo ndani ya Serikali ni kutazama kama sera na sheria tulizonazo zitakwenda kujibu matatizo ya wafanyakazi kama wa migodini kutokupata ama kupata fao la kujitoa kwa

kuzingatia *nature* ya kazi zao. Haya yote yataongozwa na mikataba ya Kimataifa na sheria tulizonazo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba nitoe wito kwa Watanzania na wafanyakazi wote watupe subira, na sisi Serikali tuko tunalifanyia kazi suala hili kwa nguvu. Nitoe onyo kwa waajiri wote wanaokiuka matakwa ya kisheria katika kuchangia mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa faida ya wafanyakazi. Na ninaomba niliarifu Bunge lako tukufu, tumeshaunda kikosi kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na tunakaribia kuanza kufanya ukaguzi wa nguvu kwa kuzingatia pia Sheria ya *Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability* na tutapambana na wale wote wanaofanya udanganyifu katika kuchangia mafao ya wafanyakazi na hasa migodini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi, Mheshimiwa Kasheku haimaniiishi watafikisha miaka 100, inachomaanisha ni kwamba wakiwa na miaka 40 atasubiri miaka 15, sio lazima afike 100. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo haya ya wafanyakazi wa migodini yamekuwa yakijirudia mara kwa mara katika Bunge hili, tumekuwa tukiyasikia, nataka kujua.

Je, ni lini sasa Serikali tafanya ukaguzi huo wa makampuni makubwa ya madini na kuwabaini wadanganyifu ambao wanakwepa kuwalipa wafanyakazi mafao yao ya *NSSF* na kodi nyingine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tumegundua kuna udanganyifu mkubwa sana katika migodi na makampuni makubwa ambayo yamekuwa yakihudumu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni hayo wakati mwingine yamekuwa yakitoa *salary slip* mbili, moja ikionesha kiwango cha chini cha malipo ya mshahara na hicho ndicho kinachofanya *contribution* kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini wana *salary slip* nyingine ambazo kodi za nchi hazikatwi inavyotakiwa wala mafao ya wafanyakazi hayapelekwi inavyotakiwa.

Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, tumegundua tatizo hilo na baada ya muda si mrefu mtasikia kikosi kazi kimeshaundwa kikiwa na wajumbe kutoka Wizara ya Fedha, *TRA*, Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya kwangu - Ofisi ya Kazi, Kamishna Mkuu na watu wengine. Watafanya ukaguzi na kuwabaini hao

wote na hatua kali zitachukuliwa na makato hayo yataanza kupelekwa kwa kuzingatia mshahara halisi wa mfanyakazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 400

**Mji Mdogo wa Mbalizi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Mbalizi uliomo kwenye Halmashauri ya Mbeya ni kati ya miji inayokua kwa kasi sana lakini inakosa miundombinu muhimu na uhaba na maji pia.

(a) Je, ni lini Mji huo utapewa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji?

(b) Je, ni lini Serikali itatatua tatizo kubwa la maji kwenye Mji huo?

(c)Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye kata zilizo ndani ya Mji wa Mbalizi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa Halmashauri za Miji nchini unazingatia Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 288 (Mamlaka za Miji) ambayo imeainisha taratibu na vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa. Hivyo, nashauri pendekezo hili lijadiliwe kwanza katika vikao vya Kamati za Maendelo ya Kata, Baraza la Madiwani na Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Endapo vikao hivyo vitaridhia, Ofisi ya Rais - TAMISEMI haitasita kuyafanyia kazi mapendekezo hayo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Mbalizi unapata maji kutoka chanzo cha Ilunga chenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 3,024 za maji kwa siku pamoja na visima kumi vya maji ambavyo vina uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 6,300 kwa siku. Mji wa Mbalizi umeingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya pili ambapo Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa

kushirikiana na Halmashauri inakusudia kuunganisha Mji huo na Mamlaka ya Maji Mkoa wa Mbeya ili kupata maji yatakayotosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mji wa Mbalizi wanapata huduma za afya kupitia Hospitali Teule ya Mbalizi pamoja na Hospitali ya Jeshi la Wananchi ambako Halmashauri imeendelea kutoa mchango wa dawa na watumishi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017, kipaumbele kimewekwa katika kukamilisha ujenzi wa zahanati nane ndani ya Halmashauri zilizoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Kwa kuwa Waziri amepotoshwa kwenye jibu (b) sehemu ya kwanza ya swali langu na hivyo kuwapotosha wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi na pia kulipotosha Bunge; je, Waziri atachukua hatua gani kwa Afisa huyo aliyempotosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ndani ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuna ardhi ya zaidi ya ekari 5,000 iliyokuwa *Tanganyika Packers,* na haijaendelezwa kwa zaidi ya miaka 30 sasa na kwa kuwa Halmashauri ya Mbeya imetenga eneo mahsusi kwa kunenepesha mfugo na kwa ajili ya kiwanda cha nyama, je, ni lini Serikali itarudisha ardhi hiyo kwa Halmasahuri ya Mbeya kwa madhumuni ya makazi bora na huduma za jamii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mkeshimiwa Oran Njeza swali lako la kwanza kama hukuridhika na majibu unatakiwa kuelekeza malalamiko yako kwa Kiti ili kijiridhishe na hayo majibu halafu kitaagiza swali lijibiwe tena, lakini sasa naona unamwambia hatua gani zitachukuliwa, Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sehemu ya kwanza nachukua kama ni maombi ya Mheshimiwa Njeza kwamba hilo swali halijajibiwa kikamilifu, na mimi nitalitolea maelezo. Endelea na swali la pili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa naomba nitoe msisitizo katika eneo la kwanza ni kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI tunapofanya hizi kazi tunahakikisha kwamba *coordination* inakamilika vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama unaona kwamba kuna mapungufu, naomba u-*clarify* ni eneo gani ambalo linaonekana halijakuwa sawasawa, ili mimi kama Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI nijue kwamba eneo gani ambalo halikukaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la opotoshaji limekuwa la jumla, lakini hili tulilielekeza katika ofisi zote za mikoa, kwamba ma-*RAS* wote wako *responsible* katika majibu yote yanayojibiwa na TAMISEMI. Kwa hiyo, nilitaka

angalau ungenipa ufafanuzi ni eneo gani uliona kwamba lilikuwa na mapungufu tuweze kulifanyia kazi kubwa, kwa sababu lengo kubwa ni kujenga, kwamba ni jinsi gani majibu yawe sawasawa kwa ajili ya kuboresha mahitaji ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika eneo la pili…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hivi swali lake kipengele (b) hakijajibiwa kabisa kwa maana hiyo, kwa sababu umepotoshwa majibu ya kipengele chote.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kuhusu swali la ni lini Serikali itarudisha eneo hili kwa ajili ya wananchi, mimi nilifika pale Mbeya nilipokwenda kutembelea Iyunga lakini nikafika katika Jimbo la Mheshimiwa. Mimi naipongeza Serikali kwa sababu kuna juhudi kubwa imefanyika, sasa pale kuna machinjio ya kisasa kwa ajili ya uchinjaji wa nyama tena wa kisasa katika eneo hilo la Mbeya. Lakini kwamba kuna eneo kubwa sasa eneo hili jinsi gani litafanyiwa kutwaliwa kurudishwa kwa wananchi kwa ajili ya makazi, nadhani sasa jambo hili ni jambo la mchakato, si jambo la kutoa maelekezo tu hapa, nini kifanyike haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu lazima tufanye tathimini ni kitu gani kilichokuwepo hapo, kwa sababu inawezekana ukienda ndani kuna migogoro mingine ya ziada. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba hilo ni suala zima la mchakato, naamini kwamba Baraza la Madiwani likikaa litafanya maamuzi litapeleka mapendekezo halafu vyombo husika vitakuja kufanya tathimini. Vitakaporidhika TAMISEMI - Ofisi ya Ardhi tutafanya tathimini ya kinakuona kama eneo hilo linaweza likarudishwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi ili wananchi wapate huduma ambayo inahitajika katika maeneo yao.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizoko wenye Mji Mdogo wa Mbalizi unafanana kabisa na changamoto zinazopatika kwenye Mji Mdogo wa Namanyere ambao pia ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi. Mamlaka hii ya Mji Mdogo wa Namanyere inahudumiwa na Mamlaka Ndogo ya Mji wa Namanyere. Mamlaka hii imeshindwa kuhudumia Mji huu kutokana na kupanuka zaidi kwa Mji wenyewe. Na kwa kuliangalia hilo Halmashauri imeshapitisha katika vikao vyake maombi ya kupata mamlaka ya Mji wa Namanyere. Je, ni lini Serikali itazingatia maombi haya ili kukidhi huduma zinazohitajika sana kwenye Mji huu wa Namanyere? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia ombi hili. Mheshimiwa Mbunge alifika ofisini kwangu na walinisaidia sana kuandaa *database* ya kuangalia maombi yote ya Miji Midogo katika Halmashauri zote za Miji mipya na Halmashauri ya Mkoa. Tunachokifanya hivi sasa ni kwamba wataalam katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI wataenda katika maeneo mbalimbali; na nilishasema mara kadhaa; baada ya kupata ile *database*, kujua nani wamefikia hatua gani, waliokidhi vigezo, na ambao hawajakidhi vigezo. Hivi tutavipata hasa baada ya wataalamu kufika *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mipata, naomba nikuhakikishie kwamba, watu wetu watafika Namanyere, watafika maeneo ya yote Sumbawanga na maeneo yale yote ambako kuna matatizo haya ya wananchi kutaka maeneo yao aidha yawe Miji Midogo, kupata Halmashauri mpya, au kupata Wilaya mpya. Wataalam wakishakamilisha lile zoezi tutakavyoangalia, pale vigezo vitakapokuwa vimefikiwa naamini Ofisi ya Rais - TAMISEMI haitosita kuipa mamlaka hii kuwa Mji Mdogo rasmi. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kutuangalia sisi kambi mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya cha Lupilo ndiyo kama Hospitali ya rufaa katika kata tano za Ilagua, Lupilo, Kichangani na Milola. Je, ni lini serikali itaifanyia ukarabati kituo hiki cha afya maana kina hali mbaya ya majengo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa sababu ni kweli kwamba Mbunge amekuja amejipanga kweli katika Bunge hili na mimi naomba nikuhakikishie, naelewa wazi kwamba ukarabati unaanza pale Baraza la Madiwani linapoweka vipaumbele. Na mimi nilivyopitia katika *database* wakati wa mchakato wa bajeti ya mwaka huu niligundua kwamba hata eneo lako la Ulanga ni kweli kuna mahitaji, isipokuwa tatizo kubwa lilikuwa katika *budget ceiling*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa zaidi naomba nikuhakikishie, ni kwamba sasa hivi ukiwasiliana na Mkurugenzi wako; kama nilivyosema siku mbili zilizopita hapa; kwamba tumewaagiza wabainishe magofu yote na maeneo yote katika eneo la afya yanayotakiwa kufanyiwa ukarabati ili Ofisi ya Rais - TAMISEMI tuangali tunapeleka wapi nguvu. Katika hilo naamini kwamba eneo lako la Ulanga katika kituo hicho cha afya ni miongoni mwa takwimu ambazo zitakuja tuweze kuzifanyia kazi. Na nikuhakikishie kwamba zitakapofika ofisini kwetu tutapanga mpango mkakati kuweza kukusaidia ili uendelee kuleta heshima katika Jimbo la Ulanga kama ilivyokuwa toka zamani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga Mbunge wa Magu sasa aulize swali lake.

Na. 401

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Zahanati za Nyang'hanga, Salongwe, Nsola, Bundilya, Nyamahanga, Nyashingwe, Chabula, Ikengele, Isangijo, Langi na Lutale ziko kwenye hatua za ukamilishaji.

Je, ni lini Serikali itazikamilisha zahanati hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Magu imetengewa shilingi milioni 160 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati kumi na tano ambazo ziko katika hatua mbalimbali. Vilevile katika mwaka 2016/2017 zimetengwa shilingi milioni 212.7 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha tunakamilisha majengo hayo ili huduma zianze kutolewa. Kama nilivyoeleza hapa Bungeni mara kadhaa, hivi sasa tunakamilisha tathmini ya ujenzi wa miundombinu ya zahanati na vituo vya afya ili kuandaa mpango wa haraka utakaosaidia kukamilisha ujenzi wa majengo hayo muhimu kwa nchi nzima.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nazidi kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kadri anavyochapa kazi kuhakikisha kwamba anatoa majibu yanayoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa kuwa zahanati hizi wananchi walizijenga, Nyang'hanga, Salongwe, Bundilya, Nsola, Nyamahanga, Nyashigwe, Chabula, Ikengele, Isangijo, Langi na Lutale; na ziko hatua za kukamilisha ili waweze kupata huduma; na kwa kuwa bajeti ya mwaka 2015/2016 inaelekea mwisho;

je, Serikali inaweza kutupatia fedha hizi kwa haraka ili tuweze kukamilisha miradi hii na wanachi wapate huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kila kijiji kiwe na zahanati, na wananchi wetu wamekuwa wakiwahi kutimiza wajibu wao kwa maana ya kujenga maboma haya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha utekelezaji wa ilani hii ili wananchi waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka kumbukumbu sawa, miongoni mwa maswali mengi niliyoyapata yalikuwa ni maswali kutoka Jimbo la Magu na miongoni mwa ziara yangu ya kwanza katika nafasi yangu Mheshimiwa Rais aliyonipa nilianza Jimbo la Magu kwa Mheshimiwa Kiswaga. Kwa hiyo. nimpongeze sana kwa kazi kubwa anayofanya na katika ziara hiyo niliona miradi mbalimbali ukiwemo mradi wa ujenzi huu wa zahanati. Naomba nikiri wazi, ni kweli fedha hazijaenda.  Lakini Serikali kama tulivyosema, kwamba tumejipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wate mnafahamu kwamba mara baada ya uchaguzi miradi mingi ilikuwa imesimama, lakini mchakato mkubwa uliofanyika kuanzia mwezi Januari mpaka tunapozungumza hivi, angalau fedha nyingi zimeenda katika miradi mbalimbali. Wakati napita kwa Mheshimiwa Kiswaga miradi mingi ilikuwa imesimama. Katika kipindi hichi Jimbo la Magu limepatiwa karibuni shilingi bilioni 4.9 baada ya msukumo mkubwa wa Serikali katika miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo najua Serikali itaendelea ku-*push* kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda. Najua katika zahanati fedha hazijaenda, lakini hata zile fedha za maji mlizokuwa mmeomba Serikali imeweza kuzipeleka kule. Hii inamaana kwamba Serikali inawajali watu wa Magu. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya juhudi zilezile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la mpango mpana wa jinsi gani maboma haya yatamaliziwa nimesema hapa mara kadhaa. Ni kwamba ni kweli jukumu letu ni kumalizia maboma. Lakini katika ajenda ya sera ya Serikali na Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi tumejielekeza kwenye vituo vya afya katika kila kata na zahanati katika kila kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Waziri wangu mwenye dhamna hapa hata jana alisema mpango wetu mpana sasa hivi ni kuhakikisha angalau kila mwaka katika Halmashauri zote tujenge kituo kimoja cha afya, lakini

halikadhalika ujenzi wa zahanati na kumalizia yale maboma. Imani yangu kubwa ni kwamba kwa sababu tuna Halmashauri 181 tukijenga kituo kimoja cha afya, maana yake tulikuwa tumejenga kwa mwaka mmoja vituo vya afya 181, ni mapinduzi makubwa kwa mwaka mmoja peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu ndani ya miaka mitano tutafanya mabadiliko makubwa, na mwisho wa siku ni kwamba Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi itatekelezeka kwa mipango hii tunaifanya pamoja baina ya TAMISEMI, Wizara ya Afya na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze na mimi kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa kuwa changamoto zinazowakabili wananchi wa Jimbo la Magu zinafanana sana na changamoto zinazolikabili Jimbo la Mbogwe, ambapo wananchi katika Kata za Ikunguigazi, Lolangulu, Ikobe na Bukwande wamejenga majengo yao ya maboma kwa ajili ya vituo vya afya lakini nguvu zao zikawa zimepelea. Je, Serikali iko tayari sasa kuwaunga mkono ili kuweza kukamlisha vituo hivyo vya afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele mjukuu wa Mzee Ulega kuwa tumeliongelea suala la zahanati na tukiwa pale Geita wakati Mheshimiwa Mama Suluhu Hassan alipokuwa akizindua hospitali kubwa ya Geita. Nimesema hapa katika majibu yangu ya msingi, kwamba mambo makubwa tunaenda kuyafanya. Sasa hivi tunafanya tathimini ili tuangalie jinsi ya gani ya kufanya.

Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Augustino kwamba tutakupa kipaumbele kikubwa zaidi na kwa sababu katika ratiba ambayo nimeitengeneza leo, katika ziara yangu miongoni mwa maeneo nitakayopita Jimbo lako nimeliweka kutokana na kunisukumasukuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukifika kule tunaweza kuangali hata *structure* ya majengo yenyewe na kukupa kipaumbe ili wanchi wako wa Jimbo la Mbogwe kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wajukuu wa Mzee Ulega tuko wengi inabidi utuorodheshe. Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kazi ya ujenzi wa zahanati ni kazi nyingine, ujenzi wa vituo vya afya ni kazi nyingine, upelekaji wa tiba ni kazi nyingine. Je, Serikali kwa sababu inajua kwamba upo upungufu mkubwa sana wa wataalam katika ngazi zote, imejipanga namna gani kuhakikisha kwamba zahanati na vituo vyote vile vinakuwa na waganga wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya mpango wa Serikali tumezungumza hapa. Ni kweli tunajenga *structures* hizi lakini lazima tupeleke vifaa tiba, dawa na wataalam. Hili tumelizungumza na mlikuwa mnajua tulikuwa na mchakato katika suala zima la ajira, lakini kutokana na changamoto ya watumishi hewa, maelekezo yametoka ya kumaliza kufanya *analysis* ya kuangalia watumishi hewa na baadaye tutaendelea na mchakato wa kupata ajira mpya na vijana wetu watapata kazi katika maeneo ya *site.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Ndassa, tuwe na subira, jambo hili linakwenda vizuri, kwa sababu vijana wanaopakuliwa kutoka vyuoni, utaratibu wa Serikali utakapokaa vizuri sasa watapelekwa maeneo husika baada ya kupata ajira ili wakawapatie wananchi huduma ya afya. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo katika swali la msingi, Wilaya ya Igunga nayo ina zahanati kama Jogohya, Mbutu, Mwazizi na Kalangale ambazo hazijakamilishwa. Je, Serikali nayo itaelekeza jicho lake huko kwenye Wilaya ya Igunga pia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu kwamba eneo lako pale, mpaka Jimbo la Manonga kwa Mheshimiwa Gulamali kuwa ni miongoni mwa eneo ambayo nimepanga kuyatembelea. Kwa sababu licha ya suala zima la umaliziaji wa zile zahanati, lakini pia kuna vituo vya afya ambavyo vimejengwa ambavyo hata upatikanaji wa vifaa vyake inaonekana kuna uchakachuaji umefanyika. Na ndio maana nimepanga ziara maalum kwa Wilaya yako ya Igunga licha ya kuangalia namna ya kumaliza zile *structure,* lakini pia kuangalia juu ya habari niliyoipata ya ubadhirifu uliofanyika katika baadhi ya maeneo. Kwa hiyo lazima nifike *site* kuja kupambana na hayo yaliyotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, na naomba nikuhakikishie kwamba wale wote ambao inaonekana wamefanya ubadhirifu katika majengo ya afya tutawachukulia hatua. Uwe na amani ya kutosha, Serikali iko kwa ajili ya kupambana na mambo ya maendeleo katika nchi yetu.

Na. 402

**Hitaji la Hospitali ya Wilaya ya Busokelo**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali itakubali kujenga Hospitali ya Wilaya ya Busokelo hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wametoa eneo tayari na wako tayari kushirikiana na Serikali?

(b) Je, kama Serikali inakubali, ni lini kazi hiyo itaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sera ya Serikali kuhakikisha tunajenga hospitali kila Wilaya, ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Utekelezaji umefanyika kupitia mpango wa Halmashauri kwa kushirikisha nguvu za wananchi, hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha Hospitali ya Wilaya inajengwa katika Halmashauri mpya ya Busokelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hospitali hiyo umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo zimetengwa shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD).*

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nimpongeze kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia suala la afya kwa Jimbo langu la Busokelo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, je, ni lini hasa hospitali hii itaanza kujengwa ikizingatia kuwa wananchi wa Jimbo la Busokelo pamoja na Mbunge wao tupo tayari kushirikiana na Serikali kujenga hospitali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na kwamba hizi shilingi bilioni mbili ambazo zimetamkwa kwenye jibu la msingi yalikuwa ni maombi maalum, je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukawathibitishia wananchi wa Jimbo la Busokelo kwamba hizi fedha sasa na maombi yao yamekubaliwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya lini hospitali hii itajengwa, nimesema hapa.

Kwanza mimi naomba niwapongeze hawa Wabunge wote unaowaona humu. Wabunge unaowaona humu jana wamefanya tukio kubwa sana la kupitisha Bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bajeti ile sasa inatupa uwezo wa kwenda kutekeleza matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikwambie sisi Mawaziri tutakuwa *serious* kuhakikisha kuwa hawa Wabunge kutokana na kelele na juhudi kubwa wanayoifanya tunawahudimia kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimueleze Mheshimiwa Mwakibete kwamba kwa sababu pesa imetengwa; na nilikuambia kwamba bajeti ya Serikali hapa imeshapitishwa, na kwamba inafanyiwa kazi; kama swali lako linavyosema fedha hii imetengwa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya yako. Jukumu letu kubwa sisi sasa ni kuweza kusimamia ili wananchi wako wapate huduma na hatimaye wa- *appreciate* kwamba wamepata Mbunge kijana wa kuwatumikia. Kwa hiyo ondoa hofu katika hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitwana Dau, Mheshimiwa Njalu naona Mheshimiwa Dau bado amekaa, labda swali lake limeshajibiwa. Mheshimiwa Njalu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa vile swali la msingi la Busokelo linafanana na la Wilaya yangu mpya ya Itilima. Kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ishatenga eneo la hekari 40 na tayari mipango yote inaendelea. Je, Serikali iko tayari kusaidia baadaye watakapokamilisha mpango huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wameshatenga eneo ekari 40, Serikali inasemaje katika hili? Serikali inachokisema ni kwamba mkimaliza mipango yenu wekeni katika Mpango wa Bajeti ya 2017/2018 kama kipaumbele cha ujenzi wa hospitali. Na ninaomba nikwambie itakapofika katika mchakato huu wa bajeti, kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa sababu sera yetu kubwa ni kujenga hospitali kila Halmashauri badala hata ya kujenga Hospitali kila Wilaya. Kwa hiyo kwa huu mpango mkiuanza sisi kazi yetu ni kusukuma tu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba uondoe hofu, ni kwamba wekeni katika mpango, nia yetu ndani ya miaka mitano watu waone kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kuleta mabadiliko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kiafya yanayoikabili Wilaya ya Busokelo yanafanana na Wilaya ya Karagwe, haina Hospitali ya Wilaya, inayo Hospitali Teule ya Nyakahanga inayotoa huduma za tiba kwa Wilaya mbili, Karagwe na Kyerwa. Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ili kuboresha huduma za afya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Karagwe hawana hospitali, lakini naomba niwapongeze kwamba wanafanya juhudi kubwa na ndiyo maana pale tumempeleka kijana mmoja anaitwa Dkt. Sobo, daktari mzuri sana wa upasuaji kama *DMO*. Ni kweli changamoto hizi, ninapata taarifa kutoka kule kila siku kwamba hakuna Hospitali ya Wilaya. Maeneo haya ni miongoni mwa maeneo tuyoyawekea kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tunajua kwamba kule mnatengeneza kikosi kazi cha kuweza kuhudumia maeneo yale, naomba katika bajeti ya mwaka unaokuja sasa wekeni kipaumbele chenu ili tuhakikishe sasa Karagwe badala ya kutumia hospitali ya *DDH,* tutumie Hospitali zetu za Wilaya kwa kuhakikisha kwamba tunaweka nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba, ikiwezekana kama kuna kituo cha afya ambacho mnatumia pale kipewe nguvu ili baadaye kipandishwe kuwa hata Hospitali ya Wilaya kwa kuanzia linaweza likawa jambo jema. Lakini naomba nikwambie kwamba, Serikali itaunga mkono juhudi zote za wana-Karagwe na watu wa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa matatizo ya Busokelo yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, na kwa kuwa, wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini tumeanzisha kwa nguvu zetu wenyewe ujenzi wa Hospitali ya Wilaya toka mwaka 2007, na mapato ya Halmashauri ni kidogo, Halmashauri imekuwa ikijenga kidogo kidogo kwa kushirikiana na wananchi wake, lakini ukamilishaji wa hospitali hii umekuwa ni mgumu.

Je, Serikali iko tayari sasa kuipa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ombi maalum la fedha ilizoomba kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Azza nakumbuka mwaka 2015 alitaka kushika shilingi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusiana na suala zima la mambo ya maendeleo katika Mkoa wa Shinyanga. Na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mwaka huu ulikuwa na kilio kikubwa sana cha suala zima la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, Serikali imesikia kilio hiki, tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo. Lengo kubwa ni kwamba, juhudi unazozifanya kwa wana-Shinyanga, kama Mbunge wao wa Viti Maalum, naomba niseme tutakuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakumbuka kuna lile ombi maalum Serikali imesikia hili. Jambo kubwa ni kwamba, tushikamane kwa pamoja tukusanye mapato, Serikali iwe na nguvu, miradi tuliyoipanga na maombi tuliyoyapeleka yote yaweze kufanikiwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Azza ondoa hofu, Serikali yako, na mimi mweyewe niseme na Waziri wangu mwenye dhamana, tuko tayari kuhakikisha kwamba Wanashinyanga wanapata huduma bora ya afya katika eneo lao. *(Makofi)*

Na. 403

**Tanzania Kufungua Ubalozi Nchini Israel**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA (K.n.y. MHE. ALLY SALEH ALLY)** aliuliza:-

Hivi karibuni Tanzania imetangaza kufungua Ubalozi wetu nchini Israel, ambapo Tanzania ilikataa uhusiano hapo nyuma.

(a) Je, ni sababu gani zilizosababisha kubadilika kwa mtazamo wa nchi na kurudisha uhusiano wa Kibalozi?

(b) Ni upi msimamo wa Tanzania katika suala la uhuru wa Palestina ambayo ndiyo iliyokuwa sababu kuu ya kukataa uhusiano na Israel hapo nyuma?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka kuwa Tanzania na Israel zilikuwa na mahusiano mazuri ya kidiplomasia mara tu baada ya Tanzania kupata uhuru, ambapo Israel ilikuwa na Ubalozi wenye Makazi yake Dar es Salaam na Tanzania ikiwakilishwa na Ubalozi wake wenye Makazi Cairo, nchini Misri. Hata hivyo, mahusiano haya yaliingia dosari kuanzia mwaka 1973 hadi 1995 kufuatiwa na maamuzi ya Umoja wa Afrika kuitenga Israel kwa sababu ya sera zake juu ya watu wa Palestina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka huo wa 1973 hadi leo mabadiliko makubwa yametokea katika medani ya Kimataifa ukijumuisha kumalizika kwa vita baridi, kusambaratika kwa Muungano wa Jamhuri ya Kisoshalisti ya Kisoviet, kuanguka kwa Ukuta wa Berlin na kuungana kwa Ujerumani Mashariki na Magharibi. Pia katika suala la mgongano kati ya Israel na Palestina kumekuwa na hatua kadhaa zinazochukuliwa kulekea kumaliza mgogoro huo pamoja na kutiwa saini kwa Mkataba wa kwanza wa Oslo wa mwaka 1995 na ule wa pili wa mwaka 1993 na 1995 na uwepo wa Mpango wa Amani wa Palestina.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1995 Tanzania ilichukua hatua ya kwenda na mabadiliko ya dunia na kuamua kuhuisha mahusiano ya kidiplomasia na Israel, ambapo kukawa na ubalozi wa Israel Tanzania mwenye makazi yake Nairobi, Kenya na Tanzania ikiwa na Balozi wa Tanzania Israel mwenye makazi yake Cairo, Misri. Aidha, mahusiano yameendelea kukua hususan baada ya Tanzania kuwa na Sera Mpya ya Mambo ya Nje ile ya mwaka 2001 inayosisitiza diplomasia ya uchumi. Kwa kutambua hatua kubwa iliyopigwa na Israel katika nyanja za kilimo, sayansi na teknolojia Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuhuisha mahusiano baina yetu ikiwa ni pamoja na kufungua Ubalozi Nchini Israel.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufungua Ubalozi wa Tanzania Israel, msimamo wa Tanzania katika kutetea haki za wanyonge Duniani, wakiwemo watu wa Palestina, bado uko pale pale kama tulivyoachiwa na muasisi wetu wa Taifa hili. Hivyo basi, msimamo wa Tanzania katika suala la Israel na Palestina ni kumaliza mzozo huu kwa amani, kwa kuwa na nchi mbili yaani Israel na Palestina huru. Kwa muktadha huo Tanzania itaimarisha mahusiano na

Israel, hususan katika mambo ya kiuchumi pamoja na kuendelea kutetea haki ya Taifa la Wapalestina kuwa huru.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kabla ya kuvunjika kwa uhusiano wetu na nchi ya Israel kulikuwa na miradi mingi ya kimaendeleo inatekelezwa, mfano Hospitali ya Bugando, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Soko la Kariakoo na miradi mingine mingi. Je, baada ya sasa kuwa tumerudisha uhusiano hali ya ushirikiano wa miaradi ya maendeleo ikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kufungua Ubalozi kwenye nchi fulani inahitajika fedha nyingi sana kuendesha. Na ndiyo hali hiyo husababisha nchi kuwa na Balozi chache au nyingi. Sasa kwa sababu, sasa hivi tuna mwendaokasi wa kufungua Balozi mpya, Israel, Kuwait, Qatar na kadhalika. Je, uwezo wetu kama nchi kwa sasa unakidhi kufungua Balozi mpya kwenye nchi nyingi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza, kwamba kabla ya mahusiano yetu kuvunjika na watu wa Israel tulikuwa na miradi mingi sana ya kimaendeleo na akihusisha mradi wa Bugando na anasema sasa baada ya kufungua hali itakuwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nimesisitiza nimesema kutokana na kwamba sasa hivi Sera za Kimataifa zimebadilika na Tanzania imeamua kubadilika. Na kwa sababu tunasisitiza Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi miradi hiyo ambayo ilikuwa imesimama wakati ule, ndiyo maana tunataka tuanzishe mahusiano haya kwa karibu ili kuweza kuendeleza miradi iliyokuwepo, lakini vilevile kufungua fursa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika suala la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge ana wasiwasi kwamba sasahivi kumekuwa na mazoea au mpango mkakati wa kufungua Balozi nyingi zaidi na ufunguzi wa Balozi unahitaji pesa nyingi. Na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyokuwa ninajibu wakati wa Bajeti kwamba Balozi hizi zitafunguliwa kutokana na uwepo wa pesa itakaokuwanao Serikali ya Tanzania. Sisi tunaelewa kwamba, ufunguzi wa Balozi ni gharama, lakini pia, gharama hiyo ya kufungua Balozi moja baada ya nyingine itategemea kwamba tutafaidika vipi katika ufunguzi wa Balozi hizo. Hatutafungua tu Balozi kwa sababu tunataka kufungua, lakini tutaangalia pia kwamba, tuna uwezo kiasi gani, kwa sababu pia ufunguzi wa Balozi unaileteea faida Tanzania. Ahsante.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa *spirit* hiyo hiyo ambayo Serikali imeiona ya kuweka mahusiano na Israel kwenye masuala ya kiuchumi, Morocco nayo vilevile iko tayari kutaka kuisaidia Tanzania kwenye masuala ya diplomasia ya uchumi. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kushirikiana na Serikali ya Morocco; najua Ubalozi upo, lakini bado Ubalozi huu haujakomaa vizuri wakati wenzetu pale Morocco wako tayari kuisaidia nchi yetu kwenye masuala ya kiuchumi wakiwa na uwezo mkubwa sana kwenye masuala ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenyewe kwamba Ubalozi wa Morocco upo na sijaelewa jinsi alivyoliweka kwamba haufanyi kazi vizuri, lakini labda pengine angetoa ufafanuzi zaidi. Lakini kwa vile nipo nitaonana nae anieleze kwamba, alikuwa na maana gani. Lakini kama kuna tatizo, sisi kama Wizara, tutalishughulikia na sisi tunajua kabisa kwamba tunafanya kazi vizuri na Morocco na kazi inasonga mbele.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema ni gharama kubwa na ni kweli ni gharama kubwa kufungua Ubalozi kamili. Na kwa kuwa, katika mahusiano ya kimataifa kuna kitu kinaitwa *Honorary Consul,* ambayo haina gharama zozote za kiuendeshaji. Je, sasa Serikali iko tayari kufungua *Honorary Consul* au Ofisi ya Uwakilishi wa Heshima huko Lubumbashi ili kusudi Tanzania iendelee kulinda maslahi yake ya kibiashara? Kwa kuwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *population* kubwa inaishi *Eastern Congo* na ndio ambayo tunafanya nayo biashara katika Miji ya Lubumbashi, Kalemie, Likasi, Kolwezi, Kisangani mpaka maeneo ya Mbujimai.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kutoka Lubumbashi mpaka kufika Kinshasha kupata huduma ni umbali wa kilometa zinazidi 2,300; yaani mtu akitoka Dar-es-Salaam atafika Lubumbashi na aliyetoka Lubumbashi hajafika Kinshasa. Kwa hiyo, hili *strategically* ni eneo zuri kibiashara.

Je, Serikali iko tayari kufungua *Honorary Consul*? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama alivyosema kwamba, je, Serikali ya Tanzania iko tayari? Anajua kwamba, kuna gharama kubwa ya kufungua Ubalozi na anashauri kwamba kwa nini tusifungue *Honorary Consul.*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimhakikishie tu Mheshimiwa Cosato Chumi, wakati kipindi hiki cha *session* za Bunge zimeanza wakati huu wa bajeti Wizara yangu pamoja Wizara kama nne hivi tumekaa tukijadili suala la mahusiano yetu kati ya sisi na Congo na Kamati zinaendelea kukaa na hili ni

moja ya ufunguzi ambao tumeliwekea mkakati. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, tunajua kwamba Lubumbashi pamoja na Kinshasa ni sehemu mbali tofauti kabisa, lakini tuna wafanyabiashara wengi sana ambao wanakwenda Congo na wanafanya biashara vizuri, ila wanapata tatizo la *coordination.* Hilo tumeliona na kazi inaendelea kufanyika.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa suala hili linahusu masuala ya Balozi; na kwa kuwa katika nchi yetu tuna Mabalozi wa CCM ambao wanafanya kazi kubwa ya kuhamasisha maendeleo, na pia kusuluhisha migogoro ambayo inajitokeza maeneo ya vijijini; je, Serikali iko tayari kuwasaidia Mabalozi hawa? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nitoe maelezo ya kushauri tu kwamba Mabalozi ninaowazungumzia mimi ni Mabalozi wa Mambo ya Nje. Lakini labda Mheshimiwa Kangi Lugola amewahusianisha hawa Mabalozi wa Mambo ya Nje kwa sababu ya mchanganyiko uliotolewa na Kambi ya Upinzani, kuwafananisha Mabalozi wa Mambo ya Nje na Mabalozi wa Nyumba Kumi Kumi. Lakini nimhakikishie tu kwamba sisi tunazungumzia Mabalozi wa Tanzania wanaotuwakilisha nje ya nchi na wanafanya kazi yao vizuri. Lakini vilevile najua kabisa kwamba, Mabalozi wa Nyumba Kumi Kumi walioko ndani ya Tanzania wanafanya kazi yao vizuri kuhakikisha kwamba masuala yanakaa salama. *(Kicheko)*

Na. 404

**Ujenzi wa Barabara ya Njombe - Makete**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO (K.n.y. MHE. LUCY M. MLOWE)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Njombe - Makete kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina iliyofanywa na Mhandisi Mshauri, *Crown Tech Consult Ltd.* kwa barabara yote ya Njombe – Ndulamo hadi Makete yenye

urefu wa kilometa 109.4 yakiwa ni maandalizi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga shilingi bilioni 19 kupitia bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Njombe - Ndulamo - Makete, na ninaomba kulishukuru Bunge lako, kiwango hiki mmekipitisha.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri juu ya barabara hii ya Njombe - Makete, lakini pamoja na barabara hii ya Njombe - Makate ndani ya Mkoa wa Njombe tuna barabara nyingine zinazounganisha na Mkoa; iko barabara ya Itoni - Ludewa inayopitia kwenye kata za Uwemba, kata ya Luponde, kata ya Matola. Na sasa hivi kule Ludewa wanaanza kulipa fidia kwa ajili ya kuanza uchimbaji wa madini, barabara hii imekuwa ikiharibika sana haioneshi kwamba kuna fedha inayotosheleza kujenga hii barabara. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambiaje sisi wana-Njombe juu ya barabara ya Ludewa - Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, alishiriki katika kuipitisha bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, na anafahamu katika bajeti hiyo tuliongea kabla na tukahakikisha tunatenga kilometa 50 za kujenga katika mwaka huu wa fedha. Na kwa sababu, bajeti imeshapitia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi yetu ni moja tu, kutekeleza eneo hilo ambalo bajeti imeipitisha. *(Makofi)*

**MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Njombe - Makete haina tofauti na barabara ya Manyoni - Itigi.

Swali, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara kilometa mbili zilizobaki kutoka njia panda inayokwenda Tabora na ile inayokwenda katikati ya Halmashauri ya Mji Mpya wa Itigi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anakumbuka katika Bunge hili hili tumejibu maswali mbalimbali na maswali ya nyongeza kuhusiana na kile kipande kidogo cha kilomita 8.3 cha kutoka Njia Panda hadi Itigi, Makao Makuu ya Halmashauri mpya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kile ambacho tulieleza wakati tunajibu swali hili hapa Bungeni; kwamba tutakapojenga ile barabara inayokwenda mpaka Rungwa, mpka Makongorosi kipande hiki kitajengwa, na unafahamu kwamba tumeshatenga fedha katika kutekeleza suala hili.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Makambako - Njombe - Songea, ilijengwa tangu mwaka 1984, na sasa ina hali mbaya sana kila siku inawekwa viraka lakini hali imekuwa ni mbaya sana.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ile upya ili kuwahudumia watu wa Mkoa wa Ruvuma na Njombe kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Makambako hadi Songea na hususani Njombe hadi Songea imetengewa bajeti ya kufanyiwa ukarabati katika mwaka huu wa fedha. Na mimi nimhakikishie ukarabati huo utakaofanyika tutahakikisha ile kampuni itakayopewa kazi hiyo ya kufanya ukarabati inafanya kwa kiwango ambacho barabara hiyo inakuwa imara na kutumika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mpakate na Wabunge wote wanahusika katika barabara hii, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Leonidas Gama ambaye alinisumbua sana ofisini kuhakikisha kwamba hili eneo linakaa vizuri ili anapopita kule asipate matatizo anayoyapata sasa. Namhakikishia na wengine wote kwamba tutahakikisha mkandarasi atakayepata kazi hii ya ujenzi ambayo bajeti mmeshaipitisha anajenga kwa kiwango kinachotakiwa.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mimi nilitaka kujua kuhusu kipande cha barabara kutoka Kibondo kwenda Mabamba kilometa 45 ambacho Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba kitajengwa kwa kiwango cha Lami. Lakini katika vitabu vyake vya bajeti imetengewa milioni 80, hiyo ni kwa ajili gani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Kibondo hadi Mabamba ilitolewa ahadi na viongozi wetu, ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Na mimi naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi hii tutaitekeleza na wala asiwe na wasiwasi. Fedha tulizozitenga za shilingi milioni 80 anazoziongelea ni kwa ajili ya ukarabati mdogo mdogo si kuanza ujenzi. Ujenzi wa kipande hiki tutaufanya kadri uwezo wa kifedha tutakapokuwa tunajaliwa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

**MHE. LOSESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda naomba ssa swali namba 104 lipatiwe majibu.

Na. 405

**Ukarabati wa Gati la Bukondo – Geita**

**MHE. LOSESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa gati la Bukondo katika Halmashari ya Wilaya ya Geita?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ninajibu swali namba 405 na naomba kujibu swali namba 405 la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari katika mwaka wa fedha 2016/2017, itafanya tafiti za eneo la gati *(Geotechnical Survey* na *Bathymetric Survey)* pamoja na usanifu wa kina *(detailed design)* kwa kutumia wataalam wa Mamlaka wa Usimamizi wa Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imepanga kuanza taratibu za kumilikishwa eneo na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa ajili ya matumizi ya bandari ikiwemo ujenzi wa Gati la Bukondo. Baada ya kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi ya Bandari itatenga fedha za ujenzi wa gati hili katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mehshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Waziri japokuwa majibu aliyonipa inaonesha kwamba ni mipango ya baadaye sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gati la Bukondo kwa sasa hivi ninavyosema liko katika hali mbaya sana kiasi kwamba watu kuvuka kwenda kupanda meli inabidi waogelee kwanza ndipo waikute meli, kwa hiyo hali ni mbaya sana. Sasa ningependa kujua Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini watakwenda kufanya ukarabati kwa sababu katika swali langu la msingi nimeuliza ukarabati wa hilo gati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Ziwa Victoria katika Halmashauri ya Ziwa Victoria pamoja na Chato tunategemea sana usafiri wa majini hasa kwa MV Chato ambayo inatoka Chato - Bukundo kwenda mpaka

Nkome. Na Nkome pia gati lake liko katika hali mbaya sana, ningependa kujua nini mkakati wa Serikali kuhakikisha ya kwamba inakarabati magati yote hayo ili wananchi waweze kupata usafiri wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba kwa namna anavyofuatilia maendeleo ya wananchi wake wa Bukwimba na wa Geita kwa ujumla. Amefika ofisini Dar es salaam na amefika vilevile Dodoma kumfuata Waziri wangu. Tumejadiliana hilo kwa kirefu na tulimuahidi kwamba tutawasiliana na wataalam wanaohusika na masuala haya ya gati ili hatimaye tuweke msukumo ili hili hitaji lake liweze kutekelezwa na wananchi wapate huduma wanayokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kurudia kile ambacho Waziri wangu alimuahidi, na mimi nilikuepo wakati anaahidiwa, na sisemi asije tena, aendelee kufuatilia, najua mambo mengi sana anafuatilia. Naomba uendelee kufuatilia, lakini kwa hili suburi tutakapokamilisha yale mawasiliano kati yetu na taasisi zinazohusika ili upate majibu sahihi na sisi tutafanya msukumo unaohitajika ili hatimaye kile kinachokusudiwa katika swali lako kiweze kukamilika.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwa kuwa gati ya Bukondo linafanana sana na kesi iliyopo kwenye gati la Nyamisati na la Kilindoni kule Mafia.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Gati la Nyamisati, na lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la abiria kwa Gati la Kilindoni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako, mimi naitwa Bwana Nyamisati. Kila ninapokutana na Mheshimiwa Dau, ndivyo anavyoniita *Mr. Nyamisati,* kwa sababu ameniambia nisipokamilisha hili ana namna, mimi sijui ana namna gani ya kuhakikisha sirudi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia tena Mheshimiwa Dau na Waheshimiwa Wabunge wengine waliokuwa wanafuatilia masuala hayo mawili pamoja na ile meli ya kutoa huduma kati Mafia na Dar es Salaam, naomba kuwahakikishieni wote, kwamba kile ambacho tumewaambia tuliwaambia tukiwa na dhamira njema. Tutahakikisha Nyamisati ambayo tayari imeshapangiwa bajeti kwa mwaka huu na mmeshaipitisha inatekelezwa. Na vilevile Kilindoni, kwa sababu tunajua Kilindoni na Nyamisati ndiyo tunakamilisha mawasiliano kati ya Mafia na upande huu wa Bara. Naomba nikuhakikishie nisingependa kuahidi kwamba tutaanza dakika hii au tutamaliza dakika hii, mimi nikuhakikishie kazi hii tutaisimamia mpaka ikamilike.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la gati lililopo katika Wilaya ya Geita linafanana kabisa na tatizo la gati lililoko katika Wilaya ya Nyasa. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Gati ya Ngumbi katika Ziwa Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nadhani ni Ndumbi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**Mheshimiwa Naibu Spika, gati linaloongelewa kama ambavyo mmeona linamuhusu sana Naibu Waziri anayehusika na masuala ya Elimu; na kwa kweli nilishuhudia mwenyewe wakati nilipoenda kukagua ile gati ambayo inatumika kupakia mkaa wa kutoka Ngaka kwamba tunahitaji kufanya mambo mazito pale ili ile biashara ambayo tayari imeshapanuka iweze kufanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, anafahamu Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kwamba katika bajeti hii ambayo nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge; na mnisamehe jana nilipa matatizo kidogo kuona kwamba mmeniwezesha kuanza kujenga reli na miundombinu mingine nikatoa kwa sauti kubwa sana kuunga mkono bajeti, nanyi mkapitisha; pamoja na hii gati ambayo ipo ina bajeti tutaisimamia kuhakikisha inakamilika na kile tunachokusudia kitendeke pale Ndumbi kiweze kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima swali fupi.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba pia niulize swali; kwa kuwa Jimbo la Kigoma Kusini kwenye Ukanda wa Ziwa Tanganyika tunatumia meli ya Liemba, lakini kwa bahati mbaya gati karibu tano kwa muda mrefu sasa hazijajengwa na wala hazijakamilika.

Swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri; je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwapunguzia adha wananchi wanaotumia meli ya Liemba kwa kujenga Gati ya Kirando, Mgambo, Sibwesa na Gati ya Kalia? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi gati anazoziongelea katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ni gati muhimu sana kwa sababu tuna vilevile tatizo la barabara. Kwa hiyo, usafiri wa ile meli ni muhimu sana kabla hatujafungua usafiri wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishawaagiza *Tanzania Ports Authority* kwamba katika mwaka huu wa fedha lazima ahadi ambazo viongozi wetu walizitoa kuanzia Serikali ya Awamu Nne na hii Serikali ya Awamu ya Tano, ni lazima tulitekeleze katika eneo hili kwa sababu mateso yaliyoko katika eneo hilo kwa kweli ni makubwa.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha na katika miaka hii mitano ikikamilika ahadi zile tutakuwa tumezikamilisha, ikiwa ni pamoja na kuimarisha gati ya Kirado, Simbwesa na hizo zingine ambazo Mheshimiwa Mbungu amezitaja.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge Maswa Magharibi sasa ulize swali lake.

Na. 406

**Bwawa la Maji Katika Kijiji cha Mwamihanza**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Bwawa la maji la Kijiji cha Mwamihanza limejaa mchanga hivyo kukauka mapema hasa ifikapo nyakati za kiangazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati bwawa hilo pamoja na miundombinu inayopeleka maji kwa wananchi wa Kijiji cha Mwamihanza na vijiji jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la maji katika Kijiji cha Mwamihanza, Wilayani Maswa lilijengwa na Serikali mwaka 1970 kwa lengo la kutoa huduma ya maji kwa wananchi na mifugo katika Kijiji cha Mwamihanza na vijiji vya jirani, na limekuwa likihudumia wakazi 1,518 na mifugo 3,578. Bwawa hili limejaa mchanga kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu zikiwemo shughuli za kilimo na mifugo eneo la *catchment* baada ya mradi wa maji kusimama kwa muda mrefu bila kufanya kazi kwa kushindwa kuendeshwa na wananchi kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bwawa la Mwamihanza ni chanzo muhimu kwa wananchi wa Kijiji cha Mwamihanza na vijiji vya jirani, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imeweka ukabarati wa bwawa pamoja na miundombinu katika mpango wa bajeti wa miaka mitatu ambapo

ukarabati utafanyika kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia vyanzo vya fedha za ndani za Halmashauri na fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali ina mpango wa kubadilisha mitambo ya kusukuma maji, inayotumia *diesel,* ili itumie nishati ya jua kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji kwa wananchi na kufanya mradi uwe endelevu. Aidha, Serikali imeanza kuvijengea uwezo vyombo vya watumia maji, ili viweze kudumu kuendesha miradi ya maji na kuifanya kuwa endelevu.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa vile bwawa hili lilikuwa likihudumia sio Kijiji cha Mwamihanza tu ni pamoja na Kijiji cha Isulilo, Kijiji cha Kidema na Kijiji cha Kulimi; na kwa vile Halmashauri na Wizara mpango wao uko mbali sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa dharura wa kuwapatia maji wananchi wa vijiji hivi, wakati tunasubiri mpango wa Halmashauri na Wizara?

Swali la pili, kwa vile pia Serikali ilishachimba mabwama mengi huko nyuma na sasa hivi mengi yao yamejaa mchanga, kama vile bwawa la Shishiu, bwawa la Jihu, bwawa la Sola, yamejaa mchanga na hivyo hayaingizi maji. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuyafufua mabwawa haya yaweze kujaa maji na kuyatunza ili wananchi wafaidike na huduma iliyokuwa ikitolewa kwenye mabwawa haya pamoja na mifugo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, bwawa hili tutalitengea fedha mwaka wa fedha 2017/2018, ni kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge ni mbali na hasa kwa kuzingatia kwamba bwawa hili linahudumia Vijiji zaidi ya vitano, katika Kata ya Kilimi, ambavyo ni Mwabayanda, Ilamata, Kulimi na Mwandu. Kwa hiyo, wananchi hawawezle kusubiri mpaka mwaka wa fedha 2017/2018. Namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, bwawa hili tutahakikisha tunatafuta fedha hata kama ni za dharura ili tuweze kulikarabati na kwa sababu mpango wa Serikali baada ya miezi sita, mwezi wa Desemba kunakuwa na marudio ya bajeti, kufanya *budget review*, basi tutahakikisha Mheshimiwa Mbunge, tunampa kipaumbele ili kuweza kuweka fedha kuhakikisha kwamba bwawa hili tunalikarabati ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ameeleza kwamba kuna mabwawa mengi ambayo yamejengwa muda mrefu, lakini mabwawa haya yamejaa mchanga na kwamba Serikali ina mpango gani kukarabati haya mabwawa. Swali la Mheshimiwa Mbunge ni zuri, lakini swali hili pia limewahi kuulizwa na

Mheshimiwa Andrew Chenge, kwamba katika maeneo yake kuna mabwawa ambayo yalijengwa zamani, yana magugu maji na yamejaa mchanga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika haya mabwawa yaliyojengwa yana matatizo makuu mawili: Moja, yanajaa michanga na pili, yanakuwa na magugu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji sasa hivi, tayari inajipanga na itaanza kufanya ukarabati kwa kuondoa magugu maji kwa kutumia njia mbili, njia moja ni njia ya kibailojia; tayari tumeshafanya mazoezi kupitia Ziwa Victoria, tuna wadudu wanaitwa mbawa kavu, ambao wakiwekwa kule wanakula yale magugu maji. Pia tutahakikisha kwamba tunaondoa mchanga kwenye haya mabwawa kwa kufanya utaratibu ambao unajulikana kama *dredging,* kuhakikisha kwamba tunapanua *capacity,* mabwawa yaendelee kupata maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo linalowakabili wananchi wa Maswa Magharibi kuhusu bwawa lao, linafanana kabisa na tatizo la bwawa la Kazima Mjini Tabora ambalo maji yake yanapungua mara kwa mara hasa wakati wa kiangazi, kutokana na tope pamoja na mchanga uliojaa pale. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha lile tope pamoja na mchanga linaweza kuondolewa ili wananchi wa maeneo yale waweze kupata maji ya kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri bwawa la Kazima nimelitembelea ni bwawa kubwa na kweli nimelikuta lina matatizo. Moja, kipindi cha kiangazi kutokana na miti mingi iliyoko kwenye lile bwawa maji yanabadilika rangi, lakini pia bwawa lile linajaa tope kutokana na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshaongea na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji wa Tabora, kuhakikisha kwamba tunashirikisha jamii. Nimwombe pia Mheshimiwa Mwakasaka, shida kubwa inayojitokeza ni kwamba wananchi wanalima sehemu ambayo maji yanatoka; baada ya kulima mvua zikinyesha zinabeba zile tope kuleta kwenye bwawa. Kwa hiyo, suala la msingi ni kwamba kwa kushirikiana na Halmashauri, tujaribu kuhakikisha kwamba tunaacha eneo la kutosha kuja kwenye bwawa, wananchi wasifanye shughuli za kilimo pamoja na ufugaji ili tuweze kulilinda bwawa letu lisijae mchanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Khamis Salum.

**MHE. SALUM K. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tatizo la bwawa la Maswa linafanana kabisa na tatizo tulilonalo katika bwawa letu la Mwenyehina Meatu na aliyekuwa Waziri wa Maji alikuja kulitembelea na akatuahidi kutusaidia chujio kwa ajili ya kusafisha maji kwa ajili ya Mji wa Mwanhuzi. Nimwombe Waziri kwa sababu ndiye aliyekuwa Naibu Waziri, atuambie bwawa hilo limefikia wapi kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona Mheshimiwa muuliza swali alichagua mtu wa kujibu, lakini nitajibu kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji Meatu, aliahidiwa kujenga chujio, katika Bunge hili tumeelekeza kwamba tumetenga fedha kupitia kwenye Halmashauri zote. Halmashauri zote 181 tumezitengea fedha na tumeelekeza kwamba, kwanza wakamilishe miradi ambayo ilikuwa inaendelea, lakini pili wahakikishe kwamba miradi ya kipaumbele kama vile kukarabati chujio ambalo Mheshimiwa Mbunge anasema, basi ni vema ashirikiane na Halmashauri kuhakikisha kwamba wanaweka kipaumbele kutumia zile fedha tulizozitenga kwa ajili ya kufanya ukarabati wa hilo eneo husika. Kama hiyo fedha itakuwa haitoshi, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane, tushirikiane ili tuangalie ni namna gani tunaweza tukaongeza fedha baada ya kufanya *budget review* mwezi wa Desemba.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia, sasa aulize swali lake.

Na. 407

**Kupanda Bei ya Dawa za Binadamu Kila Wakati**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Bei ya dawa za binadamu imekuwa ikipanda kila wakati na Serikali imekaa kimya wakati wananchi wake wanaumia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha chombo maalum cha kudhibiti bei ya dawa za binadamu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli dawa za binadamu huwa zinapanda mara kwa mara kutokana na ukweli kwamba asilimia 80 ya mahitaji ya dawa yananunuliwa kutoka nje ya nchi. Pale ambapo sarafu yetu inaposhuka thamani, au sarafu ya dola inapopanda, basi bidhaa mbalimbali toka nje ya nchi zikiwemo dawa hupanda bei. Ili kudhibiti upandaji wa bei za dawa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda, tunaandaa mkakati wa kuongeza uzalishaji wa dawa ndani ya nchi ili angalau kukidhi asilimia 60 ya mahitaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia inaangalia uwezekano wa kuunda chombo cha kusimamia gharama na bei zinazotozwa na vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na bei za dawa na vifaa tiba. Vile vile bohari ya dawa imeandaa mipango ya kuanza kununua dawa moja kwa moja, toka kwa wazalishaji ili kudhibiti bei za dawa na kuongeza upatikanaji wake, kwa bei nafuu. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati mikakati hii ya kudhibiti bei za dawa inaendelea kutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, lakini kabla ya hayo kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Dada yangu na Shemeji yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake, pamoja na Wizara nzima kwa hatua za haraka walizochukua baada ya ugonjwa wa hatari kuibuka kule Wilayani Chemba, kwa kweli nawashukuru sana na wanafanya kazi yao vizuri sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, bei ya dawa za binadamu hasa kwenye maduka ya watu binafsi imekuwa ni kubwa mno, kiasi kwamba watu wenye kipato cha chini wanashindwa kumudu gharama. Je, chombo hicho cha kudhibiti dawa kitaundwa lini?

Swali la pili, katika maduka mengi ya dawa, hasa vijijini dawa nyingi hazina ubora, lakini nyingi zinauzwa zikiwa tayari muda wake wa matumizi umekwisha na inawezekana wananchi wetu wengi wanatumia dawa hizi zikiwa

tayari zime-*expire*. Je, Serikali hili inaliona? Kama inaliona inachukua hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Kwanza nimpe pole kwa kupatwa na madhila ya ungonjwa wa hatari ambao ume-*claim* maisha ya watu kwenye Jimbo lake, lakini Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo kama ambavyo yeye mwenyewe amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni lini chombo hicho kitaanzishwa, bado tuko kwenye mchakato wa kutazama aina ya chombo ambacho tunakihitaji na namna ambavyo kitafanya kazi na pindi tutakapokamilisha utaratibu huo wa muundo wa chombo chenyewe na majukumu ya chombo hicho, kwamba yatakuwa ni yapi, ndipo tutaweza kusema ni lini chombo hicho kitaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea zina vyombo vya namna hiyo, kutokana na mifumo ya ku-*finance* mfumo wa afya kwa ujumla, zinaitwa *health technology assessment* na zinakuwa chini ya Wizara ya Afya, na sisi tumeona tuanzishe chombo kama hicho. Hivyo lini ni pale ambapo tutakamilisha utaratibu wa ndani wa utafiti kwamba tunahitaji chombo cha namna gani, chenye muundo upi na majukumu yapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kwamba dawa saa nyingine zinakuwa zime-*expire* muda wake. Hili sidhani kama linaweza likajitokeza kwa kiasi kikubwa kwenye nchi yetu; kwa sababu Mamlaka ya Chakula na Dawa wakishirikiana na Kitengo cha Ukaguzi, kilichopo chini ya Wizara ya Afya, pia wakifanya kazi kwa ukaribu na Baraza la Madawa (*Pharmacy Council)* kwa ujumla wake, huwa tunafanya ukaguzi wa kushtukiza na pia tunafanya ukaguzi maalum wa Taasisi zote ambazo zinauza dawa ama zinatoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi ule tunaweza kubaini ni dawa kiasi gani zime-*expire* na nani anayeuza dawa ambazo zime-*expire* na huwa zinawekwa chini na zinawekwa sehemu maalum na zinakuwa *labelled* kwamba zime-*expire*. Kwa maana hiyo haziwezi kuuzwa kwa wananchi. Kwa maana nyingine ni kwamba dawa ambayo *shelf life* yake ime-*expire* haiwezi kuwepo kwenye *shelf*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vifo vya wanawake wanapokwenda kujifungua katika mikoa yetu tunaposomewa, kwenye *RCC* bado iko juu sana na tena kwa muda mrefu sasa na hii ni kutokana na kukosa vifaa tiba, vitendanishi na huduma stahiki kwa ajili ya kujifungua. Je, sambamba na ukarabati wa zahanati na vituo vya afya sasa hivi kama mkakati wa Serikali, nini kauli ya Serikali hasa kutokana na vifo hivi, takwimu hizi ambazo zipo kwa muda mrefu, mama kwenda kujifungua anafariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwenye Bajeti ya mwaka huu ambapo tumetenga takribani shilingi bilioni 183, mahsusi kwa ajili ya kununua dawa na vifaatiba, nina hakika kwenye mwaka huu wa utekelezaji utakaoanza Julai Mosi, mambo yatabadilika sana kwenye sekta ya afya, hususan kwenye eneo la dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi na hivyo nimtoe shaka Mheshimiwa Umbulla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake niseme tu kwamba matatizo na changamoto ambazo zinawapata akinamama wajawazito na watoto, kipindi kile cha *puerperium* cha kujifungua na cha kunyonyesha, yatatatuliwa tu endapo tutafanya mabadiliko makubwa kwenye mfumo mzima wa afya, hususani kuwekeza zaidi kwenye mfumo wa afya ya msingi, kwa maana ya kuziwezesha zahanati na vituo vya afya ziweze kufanya kazi ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa matatizo ya bei za dawa yanaonekana yako maeneo ya mengi na kwa sababu tayari Serikali kupitia Wizara ya Afya imeanzisha maduka ya madawa *MSD* kwenye Hospitali zetu za Mkoa. Je, Serikali ina mpango gani sasa kupeleka maduka haya kwenye hospitali za Wilaya, kwa sababu ndiko kwenye watu wengi zaidi, lakini pia inaonekana ndiyo maduka yanayosaidia zaidi kwa dawa za gharama nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, sisi kama Wizara ya Afya na Taasisi yetu ya Bohari ya Taifa ya Dawa, hatuna jukumu la kuuza dawa moja kwa moja kwa wateja kwa mujibu wa sheria iliyopo na kwa maana hiyo tumefuata maelekezo ya Kiongozi Mkuu wa nchi yetu kufungua maduka ya mfano katika Hospitali ya Taifa na Hospitali za Kanda na tutaishia hapo, naomba hili kwanza lieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mkakati wa kuyawezesha maduka ya Mikoa na Wilaya, ambayo yatatamani kuwa na maduka yanayofanana na yale ya *MSD Community Outlets,* kwenye maeneo yao, lakini yale maduka watayamiliki wao, watayaendesha wao. Sisi tutawasaidia ufundi *(technical expertise),* tutawasaidia namna ya kuyajenga, kuyakarabati kwamba yanatakiwa yakae vipi, tutawasaidia mifumo ya *computer* kwa ajili ya kuendeshea biashara hiyo ya kuuza dawa; na tutawasaidia *expertise* kwamba wafanyeje *customer care* yao ili yafanane kutoa huduma katika mfumo ule ambao tunatoa kwenye maduka ya *MSD Community Outlets.* Hata hivyo, chanzo hiki cha mapato kizuri na cha uhakika kwenye hospitali za Wilaya, hatuwezi kukiondoa kwenye hospitali za Wilaya tukakileta Serikali Kuu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, Mheshimiwa Waziri, katika gazeti la Mwananchi la leo imeandikwa kwamba dawa zote zinazotakiwa wagonjwa wapate kuanzia leo au kuanzia mwaka huu zitakuwa zinalipiwa. Sasa tunatambua kwamba kuna mpango wa Serikali hasa katika dawa za watu wenye UKIMWI, Kifua Kikuu na baadhi ya magonjwa, kwamba dawa hizi zinatolewa bure. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri atuambie; je, hizi taarifa zilizotolewa leo kwenye gazeti ni za kweli? Kwanza, lakini pili kama zina ukweli ni dawa gani ambazo kuanzia sasa zitakuwa zinachajiwa, kwa maana ya kutoa pesa na dawa gani ambazo zitakuwa bure? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe shaka yeye, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba pengine gazeti hilo litakuwa limekosea tu, limefanya *misconception* ya kilichosemwa pale Muhimbili. Sijalisoma binafsi, lakini kama Naibu Waziri kwenye Wizara ambayo inasimamia utekelezaji wa Sera ya Afya natoa maelezo yafuatayo:-

Kwamba hatujabadilisha sera ya kuwahudumia Watanzania kwenye eneo la kugharamia dawa. Kwa maana hiyo utaratibu ni ule ule, hakuna dawa za UKIMWI zitakazouzwa, hakuna dawa za Kifua Kikuu zitakazouzwa, hakuna mama mjamzito wala mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano ama mzee mwenye umri zaidi ya 60 atakayeuziwa dawa, hiyo ndiyo Sera ya Afya kwenye mambo ya gharama. Kwa hiyo, kama gazeti limeandika hivyo pengine limem-*miss quote* aliyekuwa ametoa kauli inayofanana na kitu cha namna hiyo, hii ndiyo kauli ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nataka kuongeza nguvu kwamba tutaitaka, maana maneno hayo yameandikwa kwenye gazeti la leo la Mwananchi, kwa hiyo tutaitaka Muhimbili ituletee maelezo rasmi. Kwa sababu sera yetu kama alivyosema Naibu Waziri dawa ni bure kwa magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa yale ambayo yamesamehewa kwa mujibu wa sera. Kwa hiyo, nikitoka hapa tunatoa maelekezo kwa Muhimbili watuletee maelekezo rasmi na tutarudisha mrejesho hapa Bungeni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 408

**Hitaji la Benki ya Wanawake Mkoa wa Songwe**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Benki nyingi nchini zimekuwa na Riba kubwa, hali ambayo inafanya wanawake washindwe kukopa kujiinua kiuchumi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Benki ya Wanawake Mkoa wa Songwe ili wanawake wajasiriamali wanufaike na mikopo hii ya riba nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Benki ya Wanawake Tanzania ni kusambaza huduma zake katika maeneo yote ya Tanzania ikiwemo Mkoa wa Songwe. Hata hivyo, azma hii inakwamishwa na mtaji mdogo wa benki hii, ndiyo maana kwa sasa imejikita zaidi katika kutoa huduma zake kwa kutumia vituo vya mikopo ambapo hadi sasa benki ina vituo 89 katika mikoa saba ukiwemo Mkoa wa Mbeya ambao hadi mwaka 2015 ulikuwa sehemu ya Mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mkakati wa Benki ya Wanawake wa mwaka 2014/2017 ni kufungua angalau matawi matatu kila mwaka. Hii itawezekana tu endapo mtaji wa benki utakuwa kama inavyotegemewa. Hivyo benki itauingiza Mkoa mpya wa Songwe kwenye mipango yake ya upanuzi wa huduma kwa mwaka 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza!

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba benki hii kwa sasa inajikita katika kutoa huduma kwa kutumia vituo vya mikopo. Sasa nataka nijue kwamba ni lini wanawake wa Mkoa wa Songwe watapata kituo angalau kimoja ili waweze kujiinua kiuchumi?

Swali la pili, kwa kuzingatia kwamba madhumuni ya uanzishwaji wa benki hii ni kuwainua wanawake wanyonge, hususan wanaoishi vijijini, ambao hawana uwezo wa kumiliki ardhi wala nyumba kama ilivyo kwa wanawake wangu wengi wa Mkoa wa Songwe, lakini masharti ya mikopo ya benki hii kimsingi hayatofautiani sana na masharti ya benki nyingine. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kurekebisha masharti haya ya mikopo ya benki ili basi wanawake wa Mkoa wa Songwe waweze kunufaika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda nimpongeze kwa kuwajali wanawake wa Mkoa wa Songwe, yeye akiwa kama Mbunge wa eneo hilo na mimi nikiwa kama Balozi wa Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni lini tutafungua angalau kituo kimoja cha mkopo kwenye Mkoa huo. Naomba nimpe taarifa kwamba tayari tuna kituo kimoja Songwe, maeneo ya Tunduma na kwamba tayari tumemwambia kwenye jibu letu la msingi kwamba tunauweka Mkoa wa

Songwe katika mpango wetu wa kufanya kazi wa mwaka 2017/2018. Hivyo mtaji utakaporuhusu basi tutaufikiria mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba na yeye atuhurumie kwa kutambua kwamba tayari benki yetu inajitanua kidogo kidogo na kwa sababu Songwe imemeguka kutoka Mkoa wa Mbeya, ambao tayari una vituo 11 vya kutolea mikopo, atuhurumie twende na maeneo mengine, kama kumwongezea basi tutamwongezea kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu masharti ya mikopo kwenye Benki ya Wanawake; tayari Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alikwishatoa maelekezo Siku ya Wanawake Duniani mwezi wa Machi mwaka huu, kwamba Benki ya Wanawake iweke utaratibu mpya wa kushusha masharti na gharama za kutoa mikopo kwa wanawake ili wanawake wenye kipato cha chini waweze kumudu gharama za kurejesha mikopo hiyo bila usumbufu wowote. Tayari maelekezo haya ya Mheshimiwa Waziri yanafanyiwa kazi na Benki yetu ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye bajeti ya mwaka huu tayari tumeweka *provision*, ambapo kutakuwa kuna fungu maalum la pesa litakalokwenda moja kwa moja kwa wanawake wenyewe, badala ya kutumika katika *administrative activities* za benki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, kumekuwa na uhitaji mkubwa wa upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu, hususan Mkoa wangu wa Iringa na Wilaya ya Mufindi tuna *Community Bank,* sasa Serikali haioni kuwa hii ni *opportunity* nzuri kufungua dirisha pale kwa Benki ya Wanawake ili wanawake wote wa Mkoa wa Iringa waweze kunufaika na hii mikopo yenye riba nafuu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Rose Tweve kwa kuendelea kuwaseme wanawake, mtu yeyote yule akiwasemea wanawake maana yake anarahisisha kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya swali lake ni kwamba, wazo hilo la kufungua dirisha kwenye benki ya *Mufindi Community Bank* pale ni zuri sana na Serikali tunalichukua. Natumia jukwaa lako hili kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake kufanya jitihada za haraka kabisa za kuweza

kutumia fursa hii ya pendekezo linalotolewa na Mheshimiwa Rose Tweve na kuangalia maeneo mengine yote nchini ambako kuna *Community Banks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuna *Meru Community Bank,* kuna *Mwanga Community Bank;* tuna uwezo wa kufanya nao ushirikiano kwa kufungua madirisha maalum ya wanawake ili tuweze kuwafikia wanawake wengi zaidi katika nchi yetu. Hivyo, wazo lake tunalichukua.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nimuulize swali dogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, toka Bunge lililopita niliiomba Serikali itufungulie dirisha dogo la Benki ya Wanawake katika Mkoa wa Tabora na kwa kuwa, Mkoa wetu uchumi wake ni duni sana, yeye anafahamu, je, yuko tayari yeye au Waziri wake kwenda Tabora na mimi au kuja Tabora kuongea na wanawake wa Tabora, kuwapa ahadi ya ukweli yeye mwenyewe, kwa sababu mimi nilishaahidiwa hapa Bungeni litafunguliwa dirisha dogo mpaka leo halijafunguliwa, ili uwaambie ni lini sasa Serikali itakuwa tayari na benki hiyo, kuwafungulia dirisha dogo wanawake wa Mkoa wa Tabora ili nao waweze kufaidika na keki hii ya Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah kwa swali lake la nyongeza na hapo naona ananitega tu kwa sababu mimi mwenyewe natokea Tabora. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni ahadi ya Serikali toka awamu iliyopita kufungua matawi Mkoani Tabora kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema, naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake Tanzania, afanye haraka sana kwenda kufungua madirisha hayo Mkoani Tabora ili kutekeleza ahadi za Mawaziri waliokuwepo kabla yetu sisi hapa Bungeni, kwa sababu Serikali inaendelea kuwepo hata kama Mawaziri wanabadilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa maswali kwa leo. Ninayo matangazo machache halafu nitayaleta kwenu mambo mawili ambayo tuliyaahirisha wakati wa kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge, nilete tangazo la kwanza la wageni waliotufikia Bungeni leo, na hawa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kundi la kwanza ni wageni 17 wa Mheshimiwa Omar Kigua Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Kilindi Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam pia ni Mwekezaji mzawa aitwaye Ndugu Kassim Lubega, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 85 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni wanafunzi 82 na Walimu watatu wa Shule ya Msingi Kisasa ya hapa Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo ambaye ni Mwalimu Almasi Jumbe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 96 wa Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu ambao ni Walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Margareth Maria Alakok, kutoka Igunga, Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Mwalimu wao Sister Consolata Clavery, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake, pamoja na wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimboni kwake, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Livingstone Lusinde ambao ni wanakwaya wa Kikundi cha Utukufu kutoka Kanisa la Mtakatifu Andrea lililopo Kijiji cha Makang'wa, Jimbo la Mtera Mkoa wa Dodoma, wameongozwa na Mheshimiwa Patrick Makang'wa ambaye ni Diwani wa Kata ya Makang'wa na ndugu Yohana Jigwa ambaye ni Mwenyekiti wa Kwaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 35 wa Waheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mbunge wa Meatu na Mheshimiwa Leah Komanya Mbunge wa Viti Maalum, Simiyu. Wageni wao hawa ni Madiwani na wapigakura kutoka Meatu, Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Ng'oboko, Mheshimiwa Pius Machungwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 84 na Mwalimu wao kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma hapa Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni mliokuja kwa ajili ya kujifunza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo limetoka utawala, mnatangaziwa kwamba Mheshimiwa Haroun Pirmohamed, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mkoani Mbeya, kwa heshima ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan anatoa sadaka ya mchele kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Watumishi wa Bunge. Kwa hiyo, kama utawala tunawaomba mpokee kwa moyo mkunjufu, *Wabillah Tawfiq*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa makofi hayo, naona kuna Wabunge wengine wanasema asimame, hawamfahamu!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali.

*(Hapa Mheshimiwa Haroun M. Pirmohamed alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Haroun. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kilo ngapi? Tujue kabisa *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma unajua hutakiwi kuongea nikiwa naongea, lakini kilo za kutosha tu, mpaka kumaliza mwezi Mtukufu na pia utabakiza na za sherehe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo utaratibu mtatangaziwa, lakini kwa wale wachache ambao watakuwepo muda huu hapa Bungeni wataambiwa ni mahali gani waupitie, naona sijaambiwa hapa, lakini umeshawasili, upo hapa maeneo ya Bunge, ila wakati mkitoka mtaambiwa kwamba sehemu gani kila mtu akachukue huo mfuko wake wa mchele. Kwa hiyo, nimeshamshukuru Mheshimiwa Haroon Pirmohamed kwa niaba yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linawahusu Wabunge wa Makanisa ya *CCT*, Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa Ibada anawatangazia kuhudhuria ibada katika Jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne, tarehe 21 Juni saa saba mchana. Anawaomba msikose.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, anawatangazia kwamba lile dodoso mlilogawiwa jana tafadhali mlirejeshe katika yale maeneo ambayo mlikuwa mmeambiwa mpeleke, lakini kwa wale mlioko Bungeni sasa hivi mnaweza hata kumkabidhi yeye Mwenyekiti yuko pale nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mawili yalijitokeza leo asubuhi wakati wa kipindi cha maswali na majibu. Nianze na suala la kwanza la Mheshimiwa Amina Mollel, ambaye alitoa taarifa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana na Ajira akijibu swali, kwamba alipotoa taarifa maneno 'wahanga' yalitakiwa yasomeke waathirika.

Waheshimiwa Wabunge, nimeitisha hapa kamusi za aina mbalimbali ili kuelewa muktadha wa hili swali na matumizi ya neno Mhanga. Lakini nikumbushe tu, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) taarifa hupewa Mbunge anayekuwa amesimama anaongea ili Mheshimiwa Mbunge anayeona taarifa anazozisema haziko sawa yule Mbunge apewe taarifa na aulizwe kama anaikubali au anaikataa.

Sasa mazingira ambayo Mheshimiwa Amina Mollel ameyaombea taarifa siyo yale mazingira yanayotajwa kwenye Kanuni hii ya 68(8). Kwa sababu jambo hilo aliliongea hapa Bungeni na limeingia kwenye *Hansard*, nalitolea ufafanuzi kwamba, haya maneno wahanga hayakutumika na Naibu Waziri, nimeitisha *Hansard*. Hayakutumika na Naibu Waziri, yalitumika kwenye swali na swali hilo lilikuwa na vipengele vitatu. Kipengele cha kwanza ndicho kilichotumia maneno hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa hili lilikuwa ni swali liliuliza, ambalo ni Na. 399 (a) lilikuwa linasema, je, Serikali iko tayari kuzuia kuingizwa nchini vitendea kazi hatarishi na kufunga migodi ambayo ina wahanga wengi wa ulemavu na magonjwa yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini. Kwa muktadha wa swali hili, maneno wahanga hayakupaswa kutumika, yalipaswa yatumike maneno waathirika kwa sababu kama nilivyowaambia, hapa nimeitisha kamusi za aina mbalimbali ili niweze kujiridhisha. *(Makofi)*

Kwa sababu ya kuokoa muda sina haja ya kuzipitia, lakini maana ya wahanga ama muhanga imetolewa kwa namna ambayo mtu anapokea yeye maumivu kwa niaba ya mtu mwingine au kwa niaba yake mwenyewe, lakini ndiyo anakuwa amejitolea. Kwa hiyo, katika mazingira haya, ni neno waathirika au mwathirika ndiyo yaliyopaswa kutumika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine lililojitokeza asubuhi ya leo ni kuhusu majibu yaliyotolewa katika swali Na. 400 la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, kipengele cha (b), ambacho ubishani umetokea katika vyanzo vya maji vilivyotajwa katika majibu, Mheshimiwa Mbunge anasema, hivyo sio vyanzo halisi na Mheshimiwa Waziri ameletewa taarifa zote ninazo hapa, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge, wote wameniletea taarifa.

Pamoja na kwamba Kanuni ya 45(3) inanielekeza mimi kutaka swali lijibiwe upya. Katika mazingira ambayo Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa ambazo ziko tofauti na ambazo Mheshimiwa Waziri anazo na yeye amezithibitisha. Mheshimiwa Waziri ameniahidi kwamba, ataenda Jimbo la Mbeya Vijijini ili akahakikishe yeye mwenyewe mazingira yaliyopo, lakini pia na taarifa zile alizopewa.

Kwa hiyo, katika mazingira hayo, Naibu Waziri kwa kuwa ataenda huko sina haja ya kuagiza swali hilo lijibiwe upya kwa sababu kila upande unaonesha taarifa ulizonazo ni sahihi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atakapokwenda huko atatuletea taarifa kamili na maelezo yapi yalikuwa sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo …

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaruhusu Mwongozo ulioombwa, lakini tukumbuke tu kwamba, mwongozo unaombwa ikiwa hakuna Mbunge anayeongea, pia Spika akiwa hajasimama kwa sababu ukiomba amesimama maana yake wote wawili mnaongea kwa wakati mmoja, jambo ambalo Kanuni haziruhusu. Kwa hiyo, tukumbuke tu mwongozo huombwa kukiwa hakuna mtu yoyote anayezungumza ikiwa ni pamoja na Spika, Mheshimiwa Nkamia mwongozo! *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na uniwie radhi kwa sababu ulikuwa unaelekea kuahirisha kikao ndiyo maana nikakukatiza. Naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo kutokana na muda wala sina sababu ya kuisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na taarifa zilizotokea wiki iliyopita kupitia Mhimili mwingine wa Dola, lakini kwa kuwa jambo lile limeshatoka sasa na ikatolewa hukumu, nadhani kama Wabunge tuna haki ya kujiridhisha na kujua maamuzi yale. Kuna mtu alimtukana Mheshimiwa Rais na akahukumiwa kwenda jela ama kulipa faini ya shilingi milioni saba huko Arusha. Alipohukumiwa alilipa nusu ya faini ile na akaambiwa aondoke akatafute pesa nyingine. Kwa kuwa, Waziri wa Sheria yuko hapa ndani na Wanasheria wapo; mimi siyo Mwanasheria, mimi ni Mwandishi wa Habari na nimesomea pia masuala ya Uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Wanasheria watusaidie kwamba hivi kumtukana Rais wa nchi halafu yule aliyemtukana anaruhusiwa atoke akatafute fedha za kuja kulipa na siku anakabidhiwa fedha zile anaita na Waandishi wa

Habari, anapokabidhiwa zile fedha na wale waliomchangia na baadhi ya Wabunge humu ndani wa Chama fulani walionesha wanamchangia fedha yule mtu ili akalipe faini. Kwa hiyo, *in one way or another* ni kwamba alitumwa na Chama hicho akamtukane Rais na walikuwa tayari kwamba wana fedha akamtukane! Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba kama huyu alithubutu na wakamlipia faini kesho atakuja mwingine, watakwenda kumlipia faini tena! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwongozo wangu, najua jambo hili halijatokea humu ndani kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, lakini ikitokea vita nje tutazungumza hapa ndani, sasa nakuomba, hii siyo dharau kwa Rais na Serikali yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako sheria inaruhusu jambo hili kufanyika? Kama mimi leo nikahukumiwa kwa kesi ya kuiba kuku, nilipe shilingi 500,000 ama niende ndani, siwezi kuruhusiwa nikatoka nikaenda kutafuta fedha! Ilikuwaje mtu huyu akaruhusiwa kwenda nje kwenda kutafuta fedha? Akachangisha? Bado akafanya harambee akaonekana kwenye vyombo vya habari na watu wanamkabidhi fedha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi kama Juma Nkamia naona ni dharau kwa Taifa letu na tunakokwenda si pazuri! Naomba mwongozo wako, ndiyo maana nikatoa angalizo kwamba, jambo hili halijatokea ndani ya Bunge, na kwa mujibu wa Kanuni zetu kwangu naliona ni jambo la dharau sana kwa Rais na Taifa letu kwa ujumla na kwa Watanzania kwa ujumla! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri wa Sheria yupo na ni Mwanasheria mzuri, Serikali itueleze ndivyo tunavyokwenda huko sasa? Naomba mwongozo wako. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kukumbuka kwamba, jana niliomba mwongozo kwa mazingira yale ya Mheshimiwa Nkamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumemaliza kazi ya Bajeti vizuri kabisa. Wakati wa kujadili mijadala ya Wizara mbalimbali, Mawaziri na Serikali waliahidi kuleta majibu ya hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi. Kazi tumemaliza, lakini mpaka sasa au mpaka kufikia jana, ni Wizara moja tu ya Nishati na Madini ndiyo iliyokuwa imeleta majibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mawazo yangu sioni dalili ya majibu kuletwa na yawezekana Mawaziri wakadhani tumesahau! Naomba mwongozo wako kwa sababu siku zinaanza kuyoyoma!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Philipo Mulugo!

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuomba mwongozo. Kanuni ni ile ya 68 (7), lakini naomba kwa sababu ya muda nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa mara kadhaa na hata jana kwa Mheshimiwa Kadutu na leo kwa Mheshimiwa Nkamia imetokea pale ambapo Kiti, Spika, Naibu Spika ama Mwenyekiti anapokuwa amesimama, lakini anaeleza maelezo na punde anataka labda kufunga Bunge ama kwenda kwenye shughuli nyingine lakini Wabunge wanakosa nafasi ya kutoa miongozo yao. Kwa hiyo, imekuwa kama vile miongozo ni kutegeshea tu hivi! Kama vile siyo Kanuni ambayo ipo kuhusu miongozo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati gani Wabunge wawe na fursa ya kuwa wametulia na hivi ni muda wa kusema kwamba wanaweza wakaanza kuuliza miongozo yao kwa sababu imekuwa kama vile ni kitu ambacho ni cha kuiba hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo!

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nasimama kupitia Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunakuja katika Bunge hili la Bajeti, kabla ya hapo ni kwamba, ulionekana umerudisha chenji shilingi bilioni sita za Bunge. Zile pesa ziliporudishwa ilisemekana kwamba, zinarudi kwa matumizi ya kutengeneza madawati. Tumepitasha Bajeti yetu jana, tumemaliza na tunaelekea ukingoni, ningependa kujua; Je, utekelezaji umefikia wapi? Na utaratibu wa Wabunge kama mlivyotuahidi kwamba madawati hayo yataletwa katika Majimbo yetu utaratibu ukoje? Ili tunapokwenda Majimboni tuweze kujua ni lini madawati hayo yanakuja ili tuweze kushiriki kupokea na kugawa madawati hayo. Naomba mwongozo kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika Bunge lililopita kabla ya tarehe 19, tulipata taarifa kwamba Wabunge wote tutagawiwa Kompyuta za mkono *(tablets)*, ukitazama kwa kweli tuliahidiwa kwamba, tutapewa tunapofika mwishoni!

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama tumepokea hotuba nyingi za Mawaziri kwenye vitabu, tumepokea vitabu vingi vya Kamati, yaani mapendekezo ya Kamati, tumepokea hotuba nyingi za Wapinzani, hapa tulipo tuna mabegi makubwa yamejaa vitabu. Kwa kweli kufanya *reference* ya kuangalia jambo fulani lililopita katika Wizara fulani inakuwa ni ngumu kidogo. Sasa tuliahidiwa na Ofisi ya Bunge, Katibu wa Bunge kwamba, kufikia mwishoni tutakuwa tumepewa Kompyuta hizo. Naomba mwongozo wako tujue wamefikia wapi kwa sababu sasa shughuli zimekwisha, tujue ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi! *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(1).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, Kanuni ya 68(1) inaongelea Utaratibu…

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo! Nataka kwenda huko halafu niende Kanuni ya 47 ili nijenge hoja yangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, endelea!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha hoja ya Mheshmiwa Juma Seleman Nkamia Alhaji, nilitaka nisimame kuhusu utaratibu na niende Kanuni ya 47 ambayo inasomeka:

"Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Juma Nkamia ikikosa kwenye mwongozo basi, naiombea nafasi hapa kwenye mjadala ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kuijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuijadili tuone kama nchi yetu imefikia mahali ambapo sehemu ya Bunge inaweza kutukanwa na mtu akatoka nje akafanya mchango kuchangisha pesa kwa ajili ya kujiokoa na adhabu aliyopewa na Mahakama ili aendelee kuwa huru na iwe yeye awe ni mfano wa viongozi wetu kutukanwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja ili Bunge lako lijadili jambo hili, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba mkae! Mheshimiwa Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuelezea kwamba, suala ambalo Mheshimiwa Juma Nkamia na Mheshimiwa Livingstone Lusinde wamelielezea ni suala zito linalomgusa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa msimamo nitakaoutoa ambao utaingia kwenye *Hansard* uwe ni msimamo ambao unazingatia hali halisi ya kilichotokea Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningekuomba uniruhusu katika kipindi hiki hiki cha Mkutano huu nitakuja na kauli na msimamo wa Serikali kuhusu hilo suala, baada ya kupokea hukumu iliyotolewa na Hakimu, maana siwezi kusema tu bila kuisoma hiyo hukumu na vilevile, kupata maoni ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili nitakachokileta hapa, kiwe ni kitu ambacho kinazingatia msimamo wa kisheria wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nianze na mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Juma Nkamia nadhani katika maelezo yake wakati akijenga hoja yake hata yeye mwenyewe amejikumbusha kwamba hoja hiyo alioileta isingepaswa kuja chini ya Kanuni ya 68(7) kwa sababu Kanuni hii inahusu mambo yaliyotokea Bungeni mapema.

Kwa sababu hata yeye amelitolea maelezo nisingependa kulifanya refu sana. Kimsingi halikupaswa kuombewa mwongozo kwa sababu halijatokea Bungeni. Lakini nadhani Mheshimiwa Waziri atalitolea maelezo kwa mujibu wa Kanuni inayoongelea Kauli za Mawaziri, kwa hiyo, ataleta hayo maelezo wakati huo atakapokuwa tayari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nkamia, hili jambo halikupaswa kuja kwa mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Kadutu naye ameomba mwongozo kuhusu majibu ya hoja za michango ya Wabunge, ambapo Mawaziri walipokuwa wakijibu walionesha kwamba, watatoa majibu mengine kwa maandishi kwa sababu muda usingetosha kujibu hoja zote. Kimsingi hata hoja hii, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hii Kanuni inayohusu mwongozo, inaongelea Mbunge

kuuliza kama jambo lililofanyika Bungeni linaruhusiwa au haliruhusiwi, ndiyo unatumia hii Kanuni ya 68(7).

Kwa hiyo, mazingira haya ya kuuliza swali kwamba majibu hayajatolewa pia halitakiwi kuombewa mwongozo, lakini kwa sababu taarifa zake na mimi huwa nahudhuria vikao kila siku, wapo Waheshimiwa Mawaziri walioahidi kwamba, watatoa siku fulani na nakumbuka mmojawapo alikuwa ni Waziri wa Nishati na Madini aliyesema siku fulani ataleta. Wengine walikuwa wakisema kabla ya kuahirisha Bunge hili na tuna wiki hii na wiki ijayo. Kwa hiyo, tuwape huo muda wa kuweza kujitayarisha, lakini pia Mheshimiwa Kadutu amewakumbusha sasa Mawaziri kwamba, mliahidi kabla Bunge halijaahirishwa kwamba, mtaleta majibu hayo. *(Makofi)*

Mwongozo mwingine umeombwa na Mheshimiwa Philip Mulugo katika jambo ambalo nilikuwa nimelisema wakati Mheshimiwa Nkamia akiomba mwongozo, mimi nikiwa nimesimama na akauliza kwamba, hili jambo limetokea leo kwa hiyo, ni sawa kuliombea mwongozo, lakini kwamba kitendo hicho alikiona pia jana mtu aliomba mwongozo nikiwa nimesimama. Hoja ya Mheshimiwa Mulugo ni kwamba, mwongozo sasa unakuwa kama ni jambo la kutegeshea, yaani unaomba mwongozo wakati gani?

Waheshimiwa Wabunge, kwa faida yetu wote maana Bunge hili litaendelea kwa vipindi vingi sana mpaka tufike mwaka 2020. Nisome hiyo Kanuni ya 68(7) inasema hivi:

"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Waheshimiwa Wabunge, ziko Kanuni nyingine ambazo zinaambatana na hii ya mwongozo na Mbunge akiwa hasemi. Ziko Kanuni zinazosema mimi nikisimama hata mtu yoyote ambaye nilimpa nafasi ya kusimama anapaswa akae. Mimi nikisimama tu watu wote mnatakiwa kukaa. Kwa sababu hiyo, mimi nikiwa naongea hawezi mtu mwingine kuwa anaongea, ndivyo Kanuni zetu zinavyosema.

Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Spika akishasimama huwezi wewe kupata nafasi ya kuongea kwa sababu anayetakiwa kuongea ni Spika. Ndiyo maana katika utaratibu ule wa kawaida, mwongozo unaombwa wakati wowote isipokuwa awe Mbunge niliyempa nafasi labda ya kuongea

hajasimama na mimi mwenyewe sijasimama. Tukisema kwamba, mwongozo utaombwa wakati Spika amesimama maana yake atakuwa anakatizwa wakati anaongea, maana Mbunge akishasema Mwongozo wa Spika tayari amemzuia Spika kuongea kile alichotaka kuongea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika mazingira hayo, tujue tu kwamba, mwongozo siyo kwa ajili ya kutegeshea, lakini kimsingi lazima tu taratibu zifuatwe maana Kiti kikishasimama lazima watu wote mkisikilize kinasema nini. Kwa hiyo, haiwezekani Wabunge wakawa wanaongea wakati Spika amesimama!

Tutakumbuka katika utaratibu wa kawaida mara nyingi miongozo huombwa baada ya matangazo kwa sababu matangazo yakishakwisha, Spika, anapokuwa anakaa anakuwa hajamwita Katibu bado, kwa hiyo, ndiyo maana muda ule mara nyingi ndiyo unaombewa miongozo. Muda mwingine kidogo inakuwa ni tabu kwa sababu Spika akisimama au Mbunge mwingine akisimama huwezi kuomba mwongozo. Kwa hiyo, maelezo ni hayo kwamba, katika utaratibu wa kawaida unakuwa baada ya matangazo kwa sababu Spika anapokuwa anakaa na hajamwita Katibu bado, ndiyo mara nyingi miongozo huombwa pale.

Waheshimiwa Wabunge, katika mazingira ambayo kipindi cha maswali na majibu kikiisha na wakati huo Bunge linaahirishwa kidogo inaleta hiyo tafsiri ya kutegea, lakini kimsingi ni hivyo, lazima Kanuni tuzizingatie.

Mwongozo mwingine umeombwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kuhusu utekelezaji umefikia wapi wa ahadi ya madawati na kwamba lini yatakuja maana Wabunge mnaelekea Majimboni na pia hoja nyingine ni kuhusu vitabu kuwa vingi sana na kwamba Waheshimiwa Wabunge mna mabegi makubwa sana yaliojaa vitabu; kompyuta zitakuja lini?

Waheshimiwa Wabunge, tunarudi pale pale, hili jambo limeombewa mwongozo na hili jambo la kutaka taarifa ambayo haitakiwi kuombewa mwongozo. Mwongozo hauhusu taarifa inayotakiwa na Mbunge. Kwa hiyo, kwa sababu hizo, majibu ya haya maswali ya Mheshimiwa Nyongo, siko nayo hapa, lakini kwa sababu ameliomba wakati wa mwongozo, hakuna mwongozo kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Livingstone Lusinde pia alisimama kuhusu utaratibu, akataja Kanuni ya 68(1) na pia akataja Kanuni ya 47.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(1) pia inaongea mazingira ambayo Mbunge anakuwa anaongea wewe unamtaka afuate utaratibu! Sasa Mheshimiwa Lusinde hii Kanuni ya 68(1) kidogo katika mazingira ya jambo

ulilokuwa unataka kueleza utaratibu haukuwepo, lakini umetupeleka kwenye Kanuni ya 47 kwamba, hili ni jambo la dharura na ukataka kutoa hoja ili hili jambo lijadiliwe na Waheshimiwa Wabunge wakasimama ili waunge mkono hoja yako. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii Kanuni ya 47 nilipata kusema kwamba, inabidi ukiisoma Kanuni ya 47 usome na Kanuni ya 48, kwa sababu Kanuni ya 48 inaweka masharti ya mambo yanayoweza kujadiliwa kama jambo la dharura. Kwa hiyo, Kanuni ya 47(4) inasema:

"Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura, halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa."

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, hoja chini ya Kanuni 47 inapotolewa, Mbunge anatakiwa kusema maneno machache tu halafu akae, Spika afanye uamuzi ili yule mtu atoe hoja ndiyo anampa dakika tano za kutoa hoja halafu hatua nyingine sasa ndiyo Wabunge kuunga mkono hoja, ndiyo utaratibu ulivyo. Kwa mujibu wa fasili ya (4), sijaridhika kwamba, hilo jambo ni la dharura na Mheshimiwa Waziri amesema atalitolea kauli hapo baadaye, basi tutasikia hiyo kauli ya Waziri wakati huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtu wa mwisho kuongea alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe na nimeshasema kwa sababu Kanuni inamruhusu wakati huo ataleta hiyo kauli itakapokuwa tayari.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi!

*(Saa 5.23 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 22 Juni, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*